# FONOLOJIA ARUDHI YA NOMINO MKOPO ZA KIKEIYO KUTOKA KISWAHILI

**KOLONGEI PURITY CHEROTICH**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2017**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa na mtu yeyote kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote.

Sahihi............................................................................Tarehe.....................................

**KOLONGEI PURITY CHEROTICH**

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi

Sahihi................................................................Tarehe..................................................

**DKT. HANNAH MWALIWA**

Sahihi...............................................................Tarehe...................................................

**DKT. PRISCA JERONO**

**TABARUKU**

Kazi hii naitabaruku kwa;

Marehemu babu yangu,

Kipkosgei Rutto Arap Tenai

Wazazi wangu wapendwa,

William Kolongei na Elizabeth Sitienei

Nyanya zangu,

Soti Rutto na Leah Barno

# SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na uwezo wa kuyakamilisha masomo yangu ya uzamili na kuikamilisha kazi hii. Nawashukuru pia wazazi wangu wapendwa William Kolongei na Elizabeth Sitienei kwa kuniwekea msingi wa kielimu, kunitia moyo na kufadhili masomo haya. Bila wao singekamilisha masomo haya.

Shukrani za dhati ziwaendee wahadhiri wangu wote walionifunza kozi ya uzamili hadi nikamaliza; Dkt. Mbatiah, Dkt. Zaja, Dkt. Buregeya, Mwalimu Mungania, Prof. Kineene wa Mutiso, Dkt. Mukhwana, Dkt. Mbuthia, Prof. Rayya, Prof. Habwe, Dkt. Olali na Prof. Abdulaziz. Shukrani zangu pia zawandea wasimamizi wangu, Dkt. Jerono na Dkt. Mwaliwa kwa kupitia na kuihakiki kazi yangu kwa wakati ufaao, kunielekeza na kuniongoza bila kuchoka. Maelekezo na ushawishi wao ulinisaidia kukamilisha kazi hii. Daima nitawashukuru.

Namshukuru mwanangu Jepkurui Victoria kwa uvumilivu wake kuwa mbali nami wakati alinihitaji nikiwa shuleni. Nawashukuru ndugu zangu Kipchumba Collins, Kiptum Tenai, Kiptoo Tenai, Jepkorir Michelle na mpwa wangu Jepkosgei Seurei kwa kunihimiza na kuniombea ili nimalize masomo haya. Mwenyezi Mungu aendelee kuwamiminia baraka zake.

Siwasahau wenzangu; Chacha, Anusu, Muna, Zipporah, Ngulamu, Ngunyi na Otwera ambao tulisoma pamoja kozi hii. Shukrani zangu ziwaendee kwa muda tuliosoma pamoja. Tulihimizana safari ilipokuwa ngumu.

Mwisho, nawashukuru jamaa na rafiki zangu wote kwa kunihimiza kukamilisha masomo haya, kuniombea na kunifadhili kifedha nyakati zilipokuwa ngumu, kwenu wote nasema asante sana.

## IKISIRI

Utafiti huu una lengo la kuchanganua fonolojia arudhi ya nomino mkopo za Kikeiyo kutoka kiswahili sanifu. Uchanganuzi umetumia nadharia ya fonolojia vipandesauti huru inayochukulia kwamba vipandesauti vinafaa kuwakilishwa katika rusu na kila rusu huwakilisha sifa tofautitofauti. Nadharia hii imetumika kuchanganua miundo ya silabi na toni katika Kikeiyo. Nadharia ya fonolojia mizani nayo imetumika kuchanganua sifa ya mkazo katika Kikeiyo. Fonolojia ya Kikeiyo ilichunguzwa kwa kuangazia mifumo ya vokali na konsonanti ambazo hukutanishwa kuunda silabi. Miundo mbalimbali ya silabi ilielezwa. Toni na silabi ni vipashio ambavyo huwekwa kwenye silabi. Iligunduliwa kuwa uzani wa silabi huathiri mahali mkazo huwekwa katika Kikeiyo. Baada ya kuchanganua fonolojia ya Kikeiyo na kulinganua na ya Kiswahili, ilionekana kwamba nomino zinapoingizwa kutoka Kiswahili hupokea sifa za kiarudhi za Kikeiyo. Miundo ya silabi inabadilika na pamoja na miundo hii, nafasi ya mkazo inasongezwa. Toni hudhihirika katika nomino mkopo tofauti na nomino hizi asilia kwa sababu Kiswahili si lugha toni.

**YALIYOMO**


UNGAMO....ii

TABARUKU .... iii

SHUKRANI....iv

IKISIRI ....v

MAJEDWALI.... viii

ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ....ix

**SURA YA KWANZA: MSINGI WA UTAFITI** ....1

1.1 Utangulizi....1

1.1.1 Lugha ya Kikeiyo....1

1.1.2 Lugha ya Kiswahili ....3

1.1.3 Fonolojia Arudhi ....4

1.2 Tatizo La Utafiti....5

1.3 Malengo ya Utafiti ....6

1.4 Maswali ya Utafiti....6

1.5 Sababu za Kuchagua Mada....6

1.6 Upeo na Mipaka....7

1.7 Udurusu wa Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ....8

1.7.1 Fonolojia Arudhi ....8

1.7.2 Lugha za Kalenjin ....11

1.8 Misingi ya Nadharia....12

1.8.1 Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru....12

1.8.2 Nadharia ya Fonolojia Mizani....17

1.9 Mbinu za Utafiti....21

**SURA YA PILI: FONOLOJIA YA KIKEIYO**....24

2.1 Utangulizi....24

2.2 Fonolojia Vipandesauti ya Kikeiyo ....24

2.2.1 Vokali za Kikeiyo....24

2.2.2 Irabu-unganifu za Kikeiyo ....27

2.2.3 Konsonanti za Kikeiyo....28

2.2.4 Uundaji wa nusu vokali za Kikeiyo ........ 32
2.3 Fonolojia Arudhi ya Kikeiyo ........ 33
2.3.1 Silabi za Kikeiyo ........ 33
2.3.1.1 Silabi Wazi ........ 33
2.3.1.2 Silabi Funge ........ 37
2.3.2 Mkazo Katika Kikeiyo ........ 41
2.3.2.1 Mkazo Katika Maneno Yenye Silabi Moja ........ 42
2.3.2.2 Mkazo Katika Maneno Yenye Silabi Mbili ........ 43
2.3.2.3 Mkazo Katika Maneno Yenye Silabi Nyingi ........ 44
2.3.3 Toni Katika Kikeiyo ........ 46
2.3.3.1 Toni Katika Nomino za Kikeiyo. ........ 46
2.3.3.2 Majukumu ya Toni Katika Kikeiyo ........ 51
2.4 Hitimisho ........ 53
**SURA YA TATU: FONOLOJIA ARUDHI YA NOMINO MKOPO ZA KIKEIYO** ........ 54
3.1 Utangulizi ........ 54
3.2 Silabi Za Nomino Mkopo za Kikeiyo ........ 54
3.3 Mkazo katika Nomino Mkopo za Kikeiyo ........ 58
3.4 Toni za Nomino Mkopo za Kikeiyo ........ 64
3.5 Hitimisho ........ 71
**SURA YA NNE: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO ........ 72**
4.1 Utangulizi ........ 72
4.2 Mahitimisho ........ 72
4.3 Mapendekezo ........ 74
**MAREJELEO ........ 76**
**KIAMBATISHO ........ 79**
Maneno Mkopo Ya Kikeiyo Kutoka Kiswahili Sanifu ........ 79

## MAJEDWALI

Jedwali 1: Utambulisho wa Vokali za Kikeiyo........................................................25
Jedwali 2: Sifa bainifu za Vokali za Kikeiyo............................................................26
Jedwali 3: Utambulisho wa Konsonanti za Kikeiyo ..................................................30
Jedwali 4: Sifa bainifu za Konsonati za Kikeiyo ......................................................31
Jedwali 5: Uwakilishi wa Toni Katika Nomino Za Umoja........................................47
Jedwali 6: Uwakilishi wa Toni Katika Nomino za Wingi .........................................50
Jedwali 7: Mabadiliko ya Silabi..................................................................................55
Jedwali 8:Mkazo Katika Nomino Zinazohesabika Katika Umoja na Wingi ..............61
Jedwali 9: Mkazo Katika Nomino Mkopo Zisizohesabika.........................................63
Jedwali 10: Toni za Nomino Mkopo za Maumbo Ya Kimsingi .................................65
Jedwali 11: Toni za Nomino Mkopo  za Kikeiyo za Maumbo ya Kisekondari...........68

## ISHARA NA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

### ISHARA

| | |
|---|---|
| [ ] | Mabano ya kifonetiki |
| / / | Uwasilishaji wa fonimu |
| { } | Mabano ya kimofolojia |
| / | Mazingira ya kifonetiki |
| $ | Mpaka wa silabi |
| σ | Silabi |
| ⟶ | Inabadilika na kuwa |
| > | Mwelekeo wa mabadiliko |
| ′ | Mkazo |
| : | Wakaa wa vokali |

### VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| F | Futi ya kimetrika |
| N | Neno |
| V | Vokali |
| K | Konsonanti |
| KV | Konsonanti - vokali |
| FVH | Nadharia ya fonolojia vipandesauti huru |
| FM | Nadharia ya fonolojia mizani |
| VVT | Vipashio vinavyobeba toni |
| IPA | International Phonetic Alphabet |
| Ms | Mwanzo wa silabi |
| Us | Upeo wa silabi |
| C | Toni ya kidatu cha chini |
| K | Toni ya kidatu cha kati |
| J | Toni ya kidatu cha juu |
| P | Toni ya kidatu kinachopanda |
| S | Toni ya kidatu kinachoshuka |

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuangazia fonolojia arudhi ya nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili. Kiswahili ni lugha ya kibantu ilhali Kikeiyo ni lugha ya Kinailoti. Utafiti wetu ulihusisha lugha hizi mbili ili kuona namna nomino zinazokopwa kutoka Kiswahili hadi Kikeiyo zinapata athari ya sifa za kiarudhi za Kikeiyo.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya fonolojia vipandesauti huru iliyoasisiwa na Goldsmith (1976), kuchanganua toni. Nadharia ya fonolojia mizani iliyoasiswa na Liberman (1975) na kuendelezwa na Goldsmith (1990), ilitumika kuchanganua jinsi mkazo unawekwa katika Kikeiyo na kisha katika nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili.

Sura hii inahusu malengo yaliyoongoza utafiti huu, tatizo lililopelekea utafiti huu kufanywa, nadharia zilizoongoza utafiti na sababu za kufanywa kwa utafiti huu. Sura hii inaonyesha pia namna data ilikusanywa nyanjani na hatua zilizofuatwa katika uchanganuzi wa data.

### 1.1.1 Lugha ya Kikeiyo

Kikeiyo ni mojawapo ya lugha za Kalenjin. Akimnukuu Kipkorir (1978), Boen (2014:3), anathibitisha kuwa hadi kufikia miaka ya 1950, hakukuwa na jina moja la kuwarejelea watu wanaozungumza lugha za Kikalenjin. Wasomi walikuja pamoja na kubuni jina Kalenjin lenye maana ya 'ninakuambia'. Ilionekana kuwa tamko hili lilikuwa na maana sawa katika lugha zote zilizojulikana kama Kinandi na watawala

wakati huo. Jina Kalenjin lilibuniwa si kwa minajili ya kiisimu bali ni katika kukidhi mahitaji ya kisiasa ya kuwarejelea watu waliozungumza lugha za Kalenjin.

Kalenjin ni lugha mojawapo ya Kinailoti. Lugha za Kalenjin zinatokana na familia ya nailoti ya kusini. Kikeiyo kina sifa zifuatazo za kiisimu kwa mujibu wa Whiteley (1974:23-24), akirejelea sifa za lugha za kinailoti:

i. Kikeiyo kina vokali kumi. Vokali hizi ni: /i/, /e/, /u/, /o/, /a/, /ɪ/, /ɔ/, /ɛ/, /ʊ/ na /ɑ/. Kwa sababu ya sifa ya wakaa, vokali zote ni ishirini ambapo vokali refu ni /i:/, /e:/, /u:/, /o:/, /a:/, /ɪ:/, /ɔ:/, /ɛ:/, /ʊ:/ na /ɑ:/.

ii. Kikeiyo ni lugha toni. Toni hudhihirika katika vokali za wakaa fupi na refu. Toni ina majukumu ya kiisimu katika Kikeiyo kama vile kutofautisha kategoria za maneno miongoni mwa majukumu mengine kama inavyoelezwa katika sura ya pili.

iii. Silabi pendwa katika Kikeiyo ni KVK na KV. Neno [*kelde:t*] "jino" kwa mfano, lina silabi mbili zenye miundo ya KVK na KV:K. Neno [*Ke:ldo*] "mguu" lina silabi mbili, moja yenye muundo wa KVK na ya pili yenye muundo wa KV. Miundo mingine ya silabi inajadiliwa katika sura ya pili.

iv. Nomino katika Kikeiyo zina maumbo mawili. Umbo la kimsingi na umbo la upili. Umbo la kimsingi ni umbo linalorejelea nomino ambayo si mahususi. Nomino [*chi:*], kwa mfano, inatumiwa kurejelea mtu yeyote ambaye hajatajwa katika muktadha. Umbo la upili [*chi:to*] linarejelea mtu mahususi katika muktadha halisi. Umbo la upili hivyo basi, hurejelea nomino zinazofahamika.

v. Kikeiyo kina muundo wa sentensi wenye mpangilio wa kitenzi-kiima-yambwa au kitenzi-yambwa-kiima. Kwa mfano, katika sentensi: *kawa mama mbaret* (mama ameenda shambani),[*kawa*] ni kitenzi, [*mama*] ni kiima na [*mbaret*] ni yambwa. Sentensi hii pia inaweza kusemwa *kawa mbaret mama.*

Nchini Kenya wanailoti wamegawika katika makundi matatu. Kuna wanailoti wa nyanda za juu ambao ni Wakalenjin, wanailoti wa maeneo tambarare kama vile Waturkana na Wamaasai na wanailoti wanaoishi kando ya ziwa Victoria na Mto Nile kama vile Waluo.

Wataalamu mbalimbali wamejaribu kuainisha lugha za Kalenjin. Towett (1975), anaainisha lugha zifuatazo za Kalenjin: Kinandi, Kipsigis, Kikeiyo, Kitugen, Kisabaot, Kimarakwet, Kipokot, Ogiek na Kisengwer. Creider (1982:125), naye anatambua lugha kumi na moja za Kalenjin ambazo ni Kipsigis, Kinandi, Kikeiyo, Kitugen, Kimarakwet, Sabiny, Kony, Pok, Pong'om, Kiterik na Kipokot. Tarus (1994) naye, anaainisha lugha tisa za Kalenjin ambazo ni Kinandi, Kikeiyo, Kipsigis, Kitugen, Kimarakwet, Kipokot, Okiek na Sabaot inayojumuisha Kony, Bongomek na Sebei. Utafiti wetu ulitumia uainishaji wa Toweett (1975).

Lugha za Kalenjin zimegawika katika kategoria tatu; lugha zinazozungumzwa Bonde la Ufa, Mlima Elgon na Pokot. Kikeiyo kinazungumzwa Bonde la Ufa hasa kaunti za Elgeyo-Marakwet na Uasin Gishu. Lugha ambazo zimefanyiwa tafiti nyingi na kuandikiwa sana ni Kipsigis na Kinandi na ndizo zinazochukuliwa kama lahaja sanifu. Kinandi kilitumika kuchapisha Biblia, vitabu vya nyimbo na sala na ndiposa inachukuliwa kama lugha sanifu zaidi. Kikeiyo hakijatafitiwa sana kikilinganishwa na Kinandi na Kipsigis.

### 1.1.2 Lugha ya Kiswahili

Kiswahili ni lugha ya Kibantu tofauti na Kikeiyo ambayo ni lugha ya kinailoti. Kiswahili kilienezwa hadi barani kabla ya ujio wa wakoloni kupitia kwa biashara, Mbaabu (1991:3-4). Ni misafara hii ya kibiashara iliyowapelekea waswahili kufika maeneo ya mabonde ya Kerio ambayo ni makaazi ya Wakeiyo. Kama

anavyothibitisha Tarus (1994:2), waswahili ndio waliotohoa neno Elgeyo, kisawe cha Keiyo, kutokana na matamshi ya Wamaasai waliowaita Wakeiyo Il-Keyu kabla ya ujio wa wakoloni. Hili ni dhihirisho la mtagusano kati ya Wakeiyo na Waswahili na hivyo basi Kiswahili kabla ya ujio wa wakoloni. Mitagusano hii iliendelezwa hata baada ya ujio wa wakoloni ambapo Kiswahili kilitumika na wakoloni kuendesha shughuli zao. Walipata Kiswahili kama tayari ni lingua franka.

Baada ya ukoloni, Kiswahili kilipewa hadhi ya juu kutokana na sera ya nchi kuhusu lugha na hili limepelekea Kiswahili kuendelea kuenezwa zaidi nchini Kenya. Kiswahili hivyo basi, kimeendelea kutagusana na lugha nyingine zenye asili ya Kiafrika. Sera ya lugha ni kuwa, Kiswahili kinafunzwa kama somo la lazima katika shule za msingi na upili, ni lugha ya kwanza rasmi na lugha ya taifa na hivyo, kinatumika kuendesha shughuli nyingi za kitawala, kidini, kibiashara na kielimu miongoni mwa shughuli nyingine. Kutokana na sera ya lugha nchini Kenya, Kiswahili kimeweza kutagusana na Kikeiyo. Kutokana na mtagusano huu, Kikeiyo kimepata athari kubwa kutoka fonolojia ya Kiswahili kama itakavyojadiliwa.

### 1.1.3 Fonolojia Arudhi

Utafiti huu ulinuia kuangazia sifa za kiarudhi za nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili. Sifa za kiarudhi kwa mujibu wa Ladefoged (1982:219), ni zile sifa za sauti zinazohusisha vipashio vilivyo vikubwa kuliko konsonanti na vokali. Sifa hizi kwa mujibu wa Firth (1934-1935), Bendor-Samuel (1966), Hyman (1975:186), Lass (1984:239) na Verma na Krishnaswamy (1989), ni sifa zinazoenea kwa zaidi ya sauti moja.

Sifa za kiarudhi ambazo tulishughulikia katika utafiti huu ni sifa za silabi, toni na mkazo. Wataalamu wengi wanachukulia sifa za toni, mkazo na wakaa kama sifa halisi

za kiarudhi kwa sababu sifa hizi hupatikana katika matamshi yote kama anavyoeleza Hyman (1975), akimnukuu Martinet (1960). Wataalamu wengine, kwa mfano, Firth (1934-1935), anatambua silabi, toni, mkazo na wakaa kama sifa za kiarudhi nao Verna na Krishaswamy (1989), wanatambua kidatu kama sifa ya kiarudhi.

## 1.2 Tatizo La Utafiti

Lugha zozote zinapotangamana lazima ukopaji utokee. Lugha asilia zimekopa na zinaendelea kukopa maneno kutoka kwa lugha nyingine. Kikeiyo kama lugha asilia kimepata haja ya kukopa kutoka Kiswahili hasa kutokana na maingiliano kati ya lugha hizi mbili. Baada ya Kikeiyo kukopa maneno, maneno hayo hutoholewa ili yakubaliane na miundo yake ya kifonolojia. Pamoja na mabadiliko hayo, kuna mabadiliko ya kiarudhi ambayo yalikuwa msingi wa utafiti wetu. Hakuna utafiti ambao umepata kufanyiwa maneno mkopo ya Kikeiyo, utafiti huu hivyo basi ulinuia kuongeza maarifa ya kiusomi katika uwanja wa fonolojia arudhi.

Kikeiyo kama lugha ya Kinailoti ni lugha ambayo ni tofauti sana na Kiswahili ambayo ni lugha ya Kibantu. Baadhi ya sifa zinazopambanua lugha hizi mbili ni kuwa Kiswahili si lugha toni ilhali Kikeiyo ni lugha toni. Kile ambacho tulitaka kubaini ni iwapo nomino zinapokopwa kutoka Kiswahili hupokea sifa ya toni.

Isitoshe, lugha zote mbili ni lugha za mkazo. Kiswahili ni lugha yenye mkazo wa mahali mahususi. Kile tulitaka kuchunguza ni namna Kikeiyo huwekea maneno yake mkazo na iwapo uzani wa silabi huathiri mahali mkazo unapowekwa. Tulibainisha sifa hii ya mkazo inavyojitokeza katika nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili. Aidha, Kulikuwa na haja ya kubaini iwapo sehemu ya mkazo inabadilika pamoja na mabadiliko ya miundo ya silabi.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuthibitisha kuwa nomino zinapokopwa katika Kikeiyo kutoka Kiswahili hupokea sifa za kiarudhi zinazopatikana katika Kikeiyo. Kutokana na lengo hili kuu, malengo mahususi yafuatayo yaliongoza utafiti huu:

1. Kuelezea fonolojia arudhi ya Kikeiyo.
2. Kubainisha iwapo miundo ya silabi ya Kikeiyo inaathiri mahali mkazo unawekwa katika nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili.
3. Kuchanganua sifa ya toni katika nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulichochewa na maswali yafuatayo ambayo tuliyajenga kutokana na malengo ya utafiti:

1. Je, fonolojia ya Kikeiyo ina sifa zipi za kiarudhi?
2. Je, miundo ya silabi za Kikeiyo huathiri mahali mkazo unawekwa katika nomino mkopo kutoka Kiswahili?
3. Je, nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili hupata sifa ya toni?

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Fonolojia arudhi ni uwanja ambao umepuuzwa japo karibuni tafiti zimeanza kufanyiwa fonolojia arudhi. Utafiti huu hivyo basi, unadhamiria kuongeza maarifa katika uwanja wa fonolojia arudhi ya maneno mkopo.

Maneno mkopo ya Kikeiyo hayajafanyiwa utafiti wowote na hili ni jaribio la kwanza. Utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa katika kuhifadhi kimaandishi sifa arudhi na hata vipandesauti vya Kikeiyo. Kama inavyokisiwa na wataalamu kama vile Crystal (2000), lugha nyingi ulimwenguni hasa zile za kiasilia zimehatarishwa na hili huenda

likapelekea lugha hizi kufa. Utafiti huu hivyo basi ni jaribio la kuhifadhi lugha hii ya kiasilia.

Utafiti huu utawafaa wanaisimu, watafiti, wanafunzi na watu wote wanaotaka kujifunza Kikeiyo ama kutafitia masuala mengine ya kiisimu ya Kikeiyo na lugha nyingine za Kalenjin.

**1.6 Upeo na Mipaka**

Tulichagua kutumia maneno mkopo kutoka Kiswahili sanifu kwa sababu, maneno kutokana na Kiswahili yanaweza kubainishwa. Hii ni tofauti na maneno mkopo kutoka lugha nyingine kama vile Kitugen, Kinandi na Kimarakwet zinazopakana na Kikeiyo.

Tulijikita katika kategoria ya nomino kwa sababu, haya ndiyo maneno yanayokopwa sana katika lugha. Arlotto (1972:187) na Bynon (1977: 231), wakimnukuu Haugen (1950), wanatambua kwamba kategoria za maneno zinazokopwa sana ni nomino kisha vitenzi na vivumishi. Maneno ya kategoria za viwakilishi, viunganishi na vihisishi hayakopwi sana. Sababu ya kukopwa nomino kwa kiasi kikubwa ni kwa sababu maneno mengi yanayoingizwa katika lugha ni yale ya majina ya vitu vipya.

Kiwango cha fonolojia kilichoshughulikiwa katika utafiti huu ni fonolojia arudhi. Vipengele vya kiarudhi vilivyochanganuliwa ni silabi, toni na mkazo kwa sababu, katika utamkaji sifa hizi hujidhihirisha. Hata hivyo, vipengele vingine viligusiwa kama vile fonolojia vipande na mofolojia ya nomino mkopo kwa sababu, sifa za kiarudhi katika maneno ndizo zilishughulikiwa.

Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni nadharia ya vipandesauti huru yake Goldsmith (1976, 1990) na nadharia ya fonolojia mizani ya Liberman (1975). Nadharia ya vipandesauti huru ilitumika kutafitia toni katika Kikeiyo na katika nomino mkopo na

pia kuchanganua miundo ya silabi za Kikeiyo. Nadharia ya fonolojia mizani ilitumika kuchunguza mkazo katika Kikeiyo na kuona namna mkazo unavyojitokeza katika nomino mkopo.

### 1.7 Udurusu wa Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Udurusu wa yaliyoandikwa ulihusisha yaliyoandikwa kuhusu fonolojia arudhi, lugha za Kalenjin na nadharia zilizoongoza utafiti huu.

#### 1.7.1 Fonolojia Arudhi

Firth (1934-1951) ndiye anachukuliwa kuwa mwanzilishi wa nadharia ya kiarudhi. Maelezo yake kuhusu silabi hasa anapogawa silabi kama zenye aina tatu; silabi za wakaa fupi, wastani na refu, yalisaidia katika kuchanganua silabi katika Kikeiyo na hasa inapochukuliwa kuwa, wakaa wa silabi huwa na mchango katika namna mkazo unavyowekwa katika neno. Anazungumzia pia masuala ya mkazo na toni. Maelezo yake kuhusu sifa hizi za kiarudhi ziliwekea msingi utafiti huu katika kuchanganua sifa hizi katika Kikeiyo na kisha katika nomino mkopo zitokanazo na Kiswahili.

Hyman (1975, 2003) anatambua aina mbili za mkazo; mkazo huru na mkazo katika sehemu mahususi. Hyman anaelezea masuala yanayoathiri mahali mkazo unapowekwa. Maelezo haya yalituongoza katika kuchunguza sifa zinazoathiri namna mkazo unavyowekwa katika Kikeiyo na kisha, kuainisha Kikeiyo kama ni lugha yenye mkazo huru au lugha yenye mkazo katika mahali mahususi.

Fox (2000) anashughulikia suala la toni. Anaangalia dhana mbalimbali muhimu katika uwakilishaji wa toni ambazo ni pamoja na ufifishaji tonijuu, ushukajitoni kihatua, na upandajitoni kihatua. Dhana hizi ni muhimu katika uchanganuzi wowote wa toni. Maelezo yake kuhusiana na haya yalitusaidia katika kuchanganua hali hizi za toni katika Kikeiyo.

Oduor (2002) anatafitia uzani wa silabi na athari yake katika fonolojia ya Kiluo. Utafiti huu ni wa manufaa kwa sababu mtafiti alitumia nadharia za fonolojia vipandesauti huru na fonolojia mizani. Nadharia hizi zilitumika katika utafiti wetu. Anachunguza pia uzani wa silabi na namna unaathiri mahali mkazo unapowekwa katika Kiluo. Kiluo, aligundua ni lugha inayozingatia uzani wa silabi wakati wa kuwekea mkazo maneno yake. Utafiti wake ulikuwa na manufaa katika utafiti wetu katika kuelewa uhusiano uliopo kati ya uzani wa silabi na mkazo katika Kikeiyo ambayo ni lugha ya Kinailoti kama kilivyo Kiluo.

Utafiti wa Wachera (2008) ulikuwa nguzo muhimu katika kutafitia toni katika Kikeiyo. Alichunguza majukumu ya toni kileksika na kiisimu katika lahaja ya Ki-Gichugu. Tofauti na utafiti wetu ni kuwa, utafiti wetu umekita katika Kikeiyo na lugha hizi mbili ni tofauti. Ki-Gichugu ni lugha ya Kibantu ilhali Kikeiyo ni lugha ya kinailoti.

Yip (2002) anazungumzia fonolojia ya toni. Katika kujadili toni, anaonyesha sifa za toni ambazo hupambanua toni na sifa nyingine za kiarudhi. Anaendelea kuchanganua sifa hizi za toni kwa kutumia nadharia ya fonolojia vipandesauti huru. Kazi hii ilikuwa muhimu katika kujadili toni ya Kikeiyo na kuwakilisha toni katika nadharia ya fonolojia vipandesauti huru.

Mutiga (2002) anatumia nadharia ya fonolojia vipandesauti huru katika utafiti wake kuchanganua masuala ya toni katika lahaja ya Mwingi, lahaja mojawapo ya Kikamba. Nadharia hii ilimsaidia kuwakilisha, kuchanganua na kuelezea toni katika lahaja ya Mwingi. Utafiti huu ulikuwa na manufaa katika utafiti wetu kwani ulitupa mwongozo katika kuchanganua masuala ya toni katika Kikeiyo.

Chege (2009) anatafitia maneno mkopo katika Kimaasai yanayotokana na Kiingereza na Kiswahili. Anaangalia mabadiliko ya kimofofonolojia ya maneno hayo yanapoingizwa katika Kimaasai. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu mtafiti ameshughulikia silabi na toni, vipengele ambavyo vimehusika katika utafiti wetu. Utafiti huu hivyo basi ulikuwa wa manufaa katika kujenga fonolojia arudhi ya Kikeiyo kwani Kikeiyo na Kimaasai ni lugha za kinailoti zinazoelekea kufanana.

Yamo (2014) anaonyesha namna lahaja ya Boro-Ukwala inavyotohoa maneno mkopo kutoka Kimarachi, Kinyala na Kiswahili. Maelezo ya kiarudhi ya toni na mkazo, yalikuwa na umuhimu katika utafiti wetu kwani lugha zote mbili, Kikeiyo na Boro-Ukwala ni lugha za kinailoti na hivyo, zenye sifa sawa za kiarudhi; zote ni lugha toni na lugha mkazo.

Mwaliwa (2014) anachunguza miundo ya silabi katika maneno mkopo ya Kiswahili yanayotokana na Kiarabu. Anaangalia uhusiano uliopo kati ya uzani wa silabi na nafasi ya mkazo katika maneno yaliyokopwa kutoka Kiarabu. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa katika utafiti wetu kwani ulituelekeza katika kuangalia uhusiano uliopo kati ya uzani wa silabi na nafasi ya mkazo katika Kikeiyo.

Kang (2010) anaangalia mabadiliko ya kiarudhi katika maneno mkopo ya lugha mbalimbali. Anatambua kuwa lugha toni huwa na mgao huria unaoonekana wazi na huweza kuhifadhi toni ya lugha chanzi bila ukinzani wa masharti asilia ya toni. Lugha mkazo kwa upande mwingine, huwa na masharti yasiyoweza kubadilika na lugha hizi zinapokopa kutoka lugha za mkazo, zitakiuka masharti ya uaminifu kwa kubadilisha mahali mkazo wa maneno asilia unawekwa. Utafiti wa Kang ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu ulitupa mwanga katika kuangalia namna sifa za kiarudhi zinavyodhihirika katika Kikeiyo tofauti na ilivyo katika Kiswahili.

### 1.7.2 Lugha za Kalenjin

Boen (2014) anafanyia utafiti nomino mkopo katika Kinandi kutoka Kiswahili na Kiingereza. Anaangalia mabadiliko ya kimofofonolojia nomino hizi hupitia zinapotoholewa katika Kinandi. Kikeiyo na Kinandi ni lugha zinazofanana sana. Maelezo ya Boen ya vipandesauti ya Kinandi yalikuwa na umuhimu katika kujenga fonolojia vipande ya Kikeiyo.

Toweett (1975) anaainisha nomino katika Kipsigis. Anatambua maumbo mawili ya nomino za Kipsigis, maumbo ya kimsingi na upili. Kikeiyo sawa na Kipsigis, kina nomino zenye maumbo mawili. Tuliangalia maumbo ya nomino na namna toni inavyojitokeza katika maumbo haya.

Creider (1982) anaangalia sifa ya toni katika Kinandi. Anaendelea pia kuainisha aina nne za toni ambazo zipo katika Kikeiyo. Kazi yake iliwekea msingi utafiti wetu katika kufafanua toni katika nomino za Kikeiyo.

Jerono (2012) anaangalia mpangilio wa maneno katika Kitugen. Katika utafiti wake anaangalia toni inavyodhihirika katika maneno ya Kitugen. Utafiti wake ulitusaidia katika uelewa wa dhana ya toni katika Kikeiyo hasa ikizingatiwa kuwa hizi ni lugha zinazofanana.

Chelimo na Randich (2014) wanaangalia fonolojia ya Kikeiyo. Wanaandikia fonolojia vipandesauti ya Kikeiyo na miundo ya silabi katika Kikeiyo. Wanatambua kuwa, mizizi ya nomino huishia toni ya kati katika maneno yanayoundwa kwa silabi moja na toni ya kati chini katika maneno yenye silabi tatu au zaidi. Mabadiliko ya toni yanafanyika maneno yanapokuwa katika wingi. Kazi hii ilikuwa na manufaa makubwa katika utafiti wetu kwani ulitusaidia kuchanganua silabi ya nomino mkopo katika Kikeiyo zitokanazo na Kiswahili.

Kandagor na Sawe (2014) wanachanganua namna Kipsigis na Kitugen zinageuza miundo ya silabi ya maneno mkopo kutoka Kiswahili. Wanajadili miundo ya silabi katika Kipsigis na Kitugen kisha kuchanganua silabi za maneno mkopo. Utafiti wao ulitufaa katika kuchanganua miundo ya silabi katika Kikeiyo.

Chelimo, Chepkirui na Kibet (2015) wanaangalia toni inavyodhihirika katika nomino za wingi katika Kikeiyo. Kazi yao ilikuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu kwani ndio msingi wa kushughulikia masuala ya toni katika Kikeiyo.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili katika kuchanganua sifa arudhi za silabi, toni na mkazo. Masuala ya toni yalishughulikiwa na nadharia ya fonolojia vipandesauti huru (FVH), iliyoasisiwa na Goldsmith (1976). Nadharia hii imeendelezwa na Hulst na Smith (1982) na Goldsmith (1990). Nadharia hii pia ilitumika kuchanganua miundo ya silabi katika Kikeiyo.

Nadharia ya fonolojia mizani (FM) iliyoasisiwa na Liberman (1975), katika tasnifu yake ya uzamifu na baadaye kuendelezwa na Liberman na Prince (1977), Hayes (1988) na Goldsmith (1990), ilitumika kuchanganua mahali mkazo unapowekwa katika silabi za Kikeiyo.

### 1.8.1 Nadharia ya Fonolojia Vipandesauti Huru

Nadharia hii iliasisiwa na Goldsmith (1976, 1990). Goldsmith alipendekeza kuwa vipengele vya kifonolojia vichukuliwe kama vipengele vilivyo huru vinapotamkwa. Licha ya vipashio hivyo kuwa huru, vinahusiana na vipengele vingine. Nadharia hii iliasisiwa kushughulikia masuala ya toni na hivyo basi toni inachukuliwa kama kipashio kilicho huru. Msingi wa nadharia hii ni kuwa, uwakilishi wa kifonolojia unahusisha vipashio huru vinavyounganishwa pamoja kwa kutumia mistari ya

uhusiano. Uwakilishi huu hufanywa katika viwango vya juu kuliko vipashio vya konsonanti na vokali.

Nadharia hii ina mihimili miwili mikuu, Massamba (2011). Mhimili wa kwanza na ambao unaongoza utafiti huu ni kuwa, vipengele vinapaswa kuwakilishwa katika rusu kwa kutumia mistari ya uhusiano na kila kipengele kinapaswa kuwa na rusu yake, Goldsmith (1990). Kila rusu huwa tofauti kutegemea sifa inayowakilisha. Katika lugha toni, toni huwakilishwa katika rusu ya toni. Vipashio vingine vinawakilishwa katika rusu nyingine tofauti na rusu ya toni.

Kila sifa yenye jukumu la kifonolojia katika lugha huwakilishwa katika rusu moja tu, Goldsmith (1990). Sifa haziwezi kuelezwa katika rusu zaidi ya moja. Katika Kikeiyo ambayo ni lugha toni, uwakilishaji wa toni kirusu ni kama ifuatavyo:

```
(1) Rusu ya fonimu   w  e r   i    t           “mvulana”
                      |  |  |  / \   |
    Rusu ya KV        K V K V  V K
                         |      \/
    Rusu ya toni         C      J
```

Goldsmith (1990), anaeleza vipashio katika rusu ya KV vinavyohusishwa na rusu ya toni kama vipashio vinavyobeba toni (VVT). Katika utafiti huu, vokali katika rusu ya KV ndizo VVT na zinahusishwa na rusu ya toni.

Goldsmith (1976), alipendekeza kanuni tatu za sharti la ukubalifu zinazothibiti mistari ya uhusiano ili kuwe na uwiano kati ya VVT na rusu ya toni. Kanuni hizo ni:

i. Kila toni ihusishwe na angalau vokali moja au kipandesauti chenye usilabi. Hulst na Smith (1982), wanasema kuwa toni zinafaa kuhusishwa kwa njia ya moja kwa moja na vokali kuanzia kushoto kuelekea kulia hadi toni au vokali ziishe. Toni zinapobakia baada ya sheria ya kushoto-kulia kutimizwa, hazifai kuhusishwa.

ii. Kila vokali au kipandesauti chenye usilabi kihusishwe na angalau toni moja. Iwapo toni ambayo haijahusishwa na vokali ina toni upande wa kulia na kushoto, lugha mbalimbali zina taratibu tofauti ya kuhusisha toni hiyo na vokali au kipandesauti chenye usilabi, Hulst na Smith (1982). Kama anavyoeleza Goldsmith (1990), kutokana na kanuni ya uhusiano, lugha inaweza kukubalia kulimbikiza toni mwishoni mwa neno na lugha isipokubalia, kunazuka toni moja ambayo haiwezi kuhusishwa na vokali yoyote.

iii. Mistari ya uhusiano isikangamane. Kanuni hii ndio kanuni msingi katika nadharia hii.

Lugha mbalimbali huwa na sheria mbalimbali zinazoweza kuathiri kanuni hizi. Lugha zinaweza kwa mfano, kuongeza mistari ya uhusiano, kuondoa mistari ya uhusiano, kubadilisha sifa ya vipashio katika rusu au kuondoa vipashio katika rusu, (Goldsmith 1990:47). Kwa hivyo, toni hudhihirika kwa namna tofauti katika lugha mbalimbali.

Hulst na Smith (1982), wanapendekeza kanuni mbili kuu za FVH. Kanuni hizi zinaongozwa na kanuni za sharti la ukubalifu. Kanuni ya kwanza, inadai kuwa vipandesauti vilivyo katika ujirani havipaswi kufanana ila vinapokuwa katika mpaka wa neno. Kwa mujibu wa haya, toni zinazofanana haziwezi kuruhusiwa kufuatana. Toni za aina hii zinapokuwa katika neno, kanuni hii inakubalia kuziwakilisha kama toni moja. Kanuni hii ilituruhusu kukutanisha toni za aina hii katika Kikeiyo. Mfano wa kihaipothesia wa kanuni hii ni:

C    C

K  V  K

Katika mfano huu, vokali inawakilishwa na toni mbili za chini zinazofanana. Kanuni hii itaunganisha toni hii ifuatavyo:

```
   C
   |
K  V   K
```

Kanuni ya pili inaonyesha uhusiano uliopo kati ya rusu ya toni na VVT katika rusu ya KV ambayo Durand (1990) kwa mujibu wa Koske (2006), anaziita kanuni za uhusiano. Kanuni hizi zinarejelea namna kanuni za uhusiano za Goldsmith (1976), zinavyofanya kazi. Kanuni hizi za uhusiano ni:

i. Vokali na toni zinahusishwa kwa namna ya moja kwa moja kuanzia kushoto hadi kulia hadi toni au vokali ziishe.
ii. Ikiwa, baada ya kanuni ya kwanza kufanywa na baadhi ya toni hazijahusishwa, toni hizo zihusishwe na vokali ya mwisho.
iii. Ikiwa, baada ya kanuni ya kwanza kufanywa na baadhi ya vokali zikakosa toni, vokali hizo zihusishwe na toni ya mwisho.
iv. Mistari ya uhusiano wakati wa kuhusisha toni na vokali hazifai kukangamana.

**Toni za Mpandashuko**

Toni za mpandushuko zinaelezwa na Hulst na Smith (1982:6), kama, toni zinazodhihirisha hali ya kubadilika. Toni hizi zinaweza kuwa za kupanda, kushuka au za kupanda na kushuka. Goldsmith (1990:39), anaeleza toni za mpandashuko kama, mfuatano wa toni za kawaida. Toni za kawaida ni toni juu, toni kati na toni chini. Nadharia hii inabashiri kuwa, toni za mpandashuko haziwezi kuwekwa kwenye vokali za wakaa fupi kwa sababu, nadharia yoyote ya vipandesauti haikubalii mfuatano wa sifa katika kipashio kimoja, (Hulst na Smith, 1982). Vokali refu huwakilishwa kama vokali mbili fupi kisha kila vokali inabeba sehemu ya sifa inayohusishwa na toni inayobadilika. Toni inayobadilika hutokana na hali kwamba, idadi ya toni ni kubwa kuliko idadi ya silabi. Vipashio vinavyodhihirisha kuwepo kwa toni zinazobadilika huwa na sifa ya [kupanda] au [kushuka].

Nadharia hii ilituruhusu kushughulikia dhana ya toni za mpandashuko katika Kikeiyo. Kwa mfano, neno [*kòítá*] "jiwe", lenye irabu-unganifu [oi] inayotamkwa kama sauti moja itawakilishwa ifuatavyo:

```
(2) k o i t a        rusu ya fonimu
    | | | | |
    K V V K V        rusu ya KV
      | |/
      C J            rusu ya toni
```

## Toni zinazoelea

Nadharia hii kwa mujibu wa Hulst na Smith (1982), ilitatua matatizo yaliyotokana na sifa ya toni, hasa mazingira ya kifonolojia, yanayopelekea vokali moja kudondolewa lakini toni ikabaki katika neno. Toni hiyo kwa mujibu wa nadharia hii, itahusishwa na silabi nyingine. Kwa mfano:

```
(3) k u  a ny ⟹ kwa ny
      |  |         |
      C  J        CJ
```

Katika mfanyiko huu unaohusisha uyeyushaji wa vokali /u/ kuwa kiyeyusho /w/, inaonekana kuwa vokali /u/ imedondoshwa lakini toni inayohusishwa nayo haipotei bali inahusishwa na vokali /a/ hivi kwamba vokali /a/ inatamkwa na toni ya kupanda.

## Rusu ya KV

Rusu hii kwa mujibu wa Goldsmith (1990:48), ina jukumu kubwa katika upangaji wa miundo ya kifonolojia kwa sababu, hushikilia vipashio katika rusu nyingine. Toni zinahusishwa na vipashio katika rusu ya KV ambayo inahusishwa na vokali. Kwa hivyo, uchanganuzi wa toni katika VVT kwenye rusu ya KV inahusishwa moja kwa moja na silabi.

Nadharia ya FVH inawasilisha vipashio vya K na V katika rusu ya KV. Rusu ya KV ina jukumu kubwa katika utafiti wetu kwa sababu toni inahusishwa na VVT katika rusu ya KV. Kwa mfano:

(4) Rusu ya fonimu č e p t o“msichana”

Rusu ya KV KVKKV

Rusu ya toni C J

Utafiti huu ulitumia nadharia ya FVH kuchanganua miundo mbalimbali ya silabi katika Kikeiyo. Hii ni kwa sababu, vipashio vya silabi vinaelezwa kwenye rusu ya KV.

### 1.8.2 Nadharia ya Fonolojia Mizani

Nadharia hii kama inavyoelezwa na Massamba (2011) iliasisiwa na Liberman (1975), katika tasnifu yake ya uzamifu. Nadharia hii baadaye iliendelezwa na Hayes (1988), na Goldsmith (1990), miongoni mwa wengine. Nadharia hii inaonyesha kuwa kuna uhusiano kati ya uzani wa silabi na mahali mkazo unapowekwa katika lugha nyingi. Uwakilishi wa mkazo unaweza kuwa kwa matumizi ya miti ya mizani au gridi ya mizani. Utafiti wetu ulitumia miti ya mizani katika uchanganuzi wa mkazo katika Kikeiyo.

Goldsmith (1990:170) anaonyesha kuwa miti na gridi ya mizani ni sawa kwa sababu:

i. Zinaonyesha kuwa uchanganuzi wa mkazo ni tofauti na uchanganuzi wa sifa nyingine za kiarudhi.


ii. Uchanganuzi wa mkazo unahusu kuonyesha silabi inayopewa nguvu wakati wa kutamka.

iii. Mdundo wakati wa utamkaji na uzani wa silabi ni sifa muhimu katika kuchanganua mkazo.

iv. Uwakilishaji wa mkazo umepangika kwa matumizi ya rusu zilizopangika kimsonge.

**Miti ya mizani**

Mfano wa mti wa mizani kutoka Goldsmith (1990:169):




Silabi ni kiambajengo muhimu katika uchanganuzi wa uamilifu wa sauti za lugha katika nadharia ya fonolojia mizani (FM), Massamba (2011:207). Lugha hupanga maneno kwa utaratibu wa silabi. Nadharia hii kwa mujibu wa Hayes (1988), inajishughulisha na upangaji wa vipandesauti katika silabi, silabi katika futi na futi katika maneno lakini muhimu sana ni silabi. Sehemu ya silabi ambayo ni muhimu sana katika silabi ni upeo unaojengwa kwa kilele na koda, (Goldsmith 1990:170). Matawi ya mizani hupangika kiuwili katika vikonyo vinavyoitwa vikonyo dada. Wakati wa utamkaji, tawi moja husikika zaidi kuliko tawi nyingine. Tawi lenye msikiko zaidi husemwa kuwa na nguvu zaidi inawakilishwa na herufi N na tawi lisilo na msikiko husemwa kuwa hafifu na inawakilishwa na herufi H.

Upangaji katika matawi kwa mujibu wa Goldsmith (1990:171), hufuata utaratibu ufuatao:


i. Viini vya silabi hupangwa katika futi
ii. Kisha futi zikaonyesha vijenzi vya neno kama katika mfano kutoka Goldsmith (1990:169), tuliokwisha kuonyesha.

Viini vya neno huchanganuliwa katika futi za mkazo hivi kwamba kila kiini sharti kiwe ni sehemu ya futi ya mkazo. Wakati futi zinajengwa inapaswa kuonyeshwa iwapo futi ni ya mwelekeo wa kushoto (kiini cha kushoto kabisa kinapokea mkazo) au mwelekeo wa kulia (kiini cha kulia kabisa kinapokea mkazo). Hiki kwa mujibu wa Goldsmith (1990:171), ni kigezo cha kwanza katika sheria za mizani, kama futi ni inayoelekea kulia au kushoto. Kiini kinachopokea mkazo kinakuwa kichwa cha futi ya mizani.


Kigezo cha pili ni mwelekeo wa upangaji wa sheria, kama futi zinajengwa kuelekea kulia kuanzia mwanzo wa neno au kulia kuanzia mwisho wa neno. Neno linapokuwa na silabi tatu au tano baada ya kujenga futi, silabi moja inabakishwa (silabi baki). Futi inajengwa kuwasilisha silabi hii mwishoni mwa neno na futi hiyo haina matawi.

Mifano kutoka (Goldsmith 1990:172), kuonyesha kigezo cha pili;

**Futi ya kulia**




**Futi ya kushoto**





**Silabi baki**





Goldsmith (1990:172), akiwanukuu Durand (1986), na Lerdahl na Jackendoff (1983), anaonyesha kuwa walitofautisha futi za kushoto na kulia kwa kuweka kikonyo

kinachowakilisha kiambajengo cha futi, juu ya kichwa kama inavyoonyeshwa ifuatavyo:

**Futi ya kushoto**




**Futi ya kulia**




**Silabi baki**





Uwakilishi huu ndio ambao ulitumika katika utafiti wetu.

Futi ambazo hazina matawi hudondolewa kwa kuzihusisha na futi iliyo jirani nayo katika neno lenye silabi mbili. Neno linapokuwa na silabi tatu, futi isiyokuwa na tawi hubadilishwa ili iwe katika ujirani na mkazo hafifu ili kuepuka hali ya kuwa na mgongano wa mkazo, Goldsmith (1990:176). Ubadilishaji wa silabi hiyo haiwezekani kwenye neno lenye silabi tano kwa sababu, kubadilisha nafasi kunaleta hali ya mgongano wa mikazo.

Kigezo cha tatu kinahusu uzani wa silabi. Muundo wa ndani wa silabi huathiri mahali mkazo huwekwa isipokuwa kwa lugha zisizozingatia uzani wa silabi katika kuwekea maneno yake mkazo, Goldsmith (1990:178). Katika sheria nyingi za mikazo, uzani wa silabi huwa na jukumu katika kuwekea neno mkazo, Hayes (1988:230) na Goldsmith (1990:177). Silabi nzito huwa na matawi katika migao yake ilhali silabi nyepesi ina tawi moja tu. Silabi nzito huhitaji kuwekewa mkazo, Goldsmith

(1990:178). Ujenzi wa futi za mkazo huhitaji silabi nzito ili kuweka mkazo mahali pafaapo.

Kigezo cha nne kinahusu mipaka ya futi. Futi moja huweza kuthibiti au kukosa kuthibiti futi nyingine, Goldsmith (1990:181). Lugha isipokubalia kikonyo kimoja kuthibiti kingine kutakuwa tu na matawi mawili lakini lugha inapokubali kikonyo kimoja kuthibiti nyingine kunakuwa na mgao kama ufuatao kutoka, (Goldsmith 1990:181):




Nadharia hii pia inaelezea kuhusu mkazo msingi. Mkazo msingi kwa mujibu wa Goldsmith (1990:183), ni msikiko wa nguvu wa futi moja ya mkazo ikilinganishwa na futi zingine.

**1.9 Mbinu za Utafiti**

Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka kijiji cha Kapkonga, kata ya Kapkwoni, kaunti ya Elgeyo Marakwet. Mtafiti aliteua eneo hili kwa sababu mbili. Sababu ya kwanza ni kuwa, wakaazi wa eneo hili ni wanaotumia Kikeiyo katika mawasiliano yao ya kila siku na kama anavyosema Milroy (1967:57), data nzuri ya lugha asilia ni ile inayotokana na wanaotumia lugha inayotafitiwa katika mawasiliano yao ya kila siku. Eneo hili lilichaguliwa pia kwa sababu ya uhusiano wa karibu kati ya mtafiti na wakaazi.

Utafiti wa kwanza ulifanywa nyanjani. Data iliyokusanywa nyanjani ni utamkaji wa nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili. Baada ya kukusanya data ya matamshi,

tulifanya utafiti wa maktabani ili kusoma yaliyoandikwa kuhusu ukopaji, lugha za Kalenjin, fonolojia arudhi na yaliyoandikwa kuhusu nadharia zinazoongoza utafiti huu.

Tulitumia kichanganuzi-kidatu cha praat inayopatikana katika www.praat.org. Praat hutumiwa kuchanganua toni. Kwanza, Sauti zilirekodiwa kisha sauti hizo zikahifadhiwa. Uchanganuzi ulihusisha kufungua sauti hizo zilizorekodiwa na kuhifadhiwa na kuangalia kwenye grafu namna kasimawimbi ya sauti hizo zilivyotokea katika mstari.

**Watafitiwa**

Watafitiwa walichaguliwa kwa misingi ya wao kuwa wazungumzaji asilia wa Kikeiyo wanaotumia Kikeiyo katika mawasiliano yao ya mara kwa mara. Tuliteua watafitiwa ishirini bila kuzingatia jinsia kwa sababu utafiti huu ulihusu kuchunguza kwa ujumla sifa za kiarudhi za nomino mkopo zilizokopwa kutoka Kiswahili.

**Data**

Tulitengeneza orodha ya nomino mkopo sabini na tisa katika Kikeiyo zinazotokana na Kiswahili. Mtafiti alitumia tajriba yake ya Kikeiyo kutambua nomino zilizokopwa kutoka Kiswahili na pia kwa kusikiliza idhaa ya redio ya KASS. Watafitiwa walipewa orodha ya maneno ya Kiswahili kusoma kwa kutumia Kikeiyo. Wale ambao hawakujua kusoma walisomewa maneno ya Kiswahili na kisha wakataja maneno hayo kwa Kikeiyo. Sauti za watafitiwa zilinaswa wakati wa utamkaji kwa kutumia kinasa sauti. Sauti hizi ndio ilikuwa data ya utafiti iliyochanganuliwa.

**Uchanganuzi wa data**

Tulikuwa na jedwali lenye sehemu tatu ya kunakili nomino kwa umoja na wingi. Baada ya kunakili nomino hizo na pia kutokana na umilisi wa mtafiti wa Kikeiyo, tuliandika nomino hizo kifonetiki.

Tulikuwa na jedwali jingine la kuonyesha mkazo katika maneno kwa umoja na wingi. Tulisikiliza kwa makini kanda huku tukibainisha mkazo unapotokea katika kila neno. Alama (′) ilitumika kuonyesha mkazo unawekewa silabi gani katika neno. Tulitumia vigezo vya nadharia ya FM kutambua mkazo unawekwa katika silabi gani.

Tulikuwa na jedwali jingine la kuchanganulia toni. Sauti zilizonaswa ziliingizwa kwenye kichanganuzi-kidatu cha praat. Tuliona kwa kila neno namna kasimawimbi inavyobadilika na kubainisha toni katika kila nomino mkopo. Tulitumia nadharia ya FVH kuchanganua sifa ya toni katika nomino hizo kopwa.

Tulifanya uchanganuzi wa toni na mkazo huku tukilinganisha na asili ya maneno haya na kuona jinsi sifa hizi zinajidhihirisha. Matokeo ya uchanganuzi yaliwasilishwa kwa maelezo na michoro matawi.

# SURA YA PILI

# FONOLOJIA YA KIKEIYO

## 2.1 Utangulizi

Lugha zozote zinapotagusana, lazima ukopaji ufanyike kama tulivyoonyesha katika sura ya kwanza. Kiswahili na Kikeiyo, kama tulivyokwisha kuonyesha ni lugha ambazo zimetagusana kwa muda mrefu na hili limepelekea Kikeiyo kukopa kutoka Kiswahili. Utafiti huu ulichunguza sifa za kiarudhi za nomino hizi. Kabla ya kuangazia fonolojia arudhi ya nomino mkopo za Kikeiyo, tulichanganua fonolojia ya Kikeiyo. Kwanza, tulionyesha mifumo ya vokali na konsonanti katika Kikeiyo. Baada ya kuangalia mifumo hii ya konsonanti na vokali, tulielezea miundo mbalimbali ya silabi za Kikeiyo kwa sababu sifa za kiarudhi zilizoshughulikiwa katika utafiti huu ni zile zinazowekwa kwenye silabi. Baada ya kuelezea silabi za Kikeiyo, tulibainisha namna miundo ya silabi hizo inaathiri mahali mkazo unawekwa katika nomino mkopo. Mwisho, tulichanganua sifa ya toni inavyodhihirika katika nomino hizi.

## 2.2 Fonolojia Vipandesauti ya Kikeiyo

Fonolojia vipandesauti inajumuisha sauti za konsonanti na vokali. Kikeiyo kina fonimu za aina hizi mbili.

### 2.2.1 Vokali za Kikeiyo


Vokali kwa mujibu wa Massamba (2004), ni sauti zinazotolewa wakati glota inaachwa wazi na hewa haitatizwi. Chelimo na Randich (2014), wanaeleza kwamba, Kikeiyo kina vokali kumi za aina mbili; vokali za wakaa fupi na vokali za wakaa refu. Vokali za wakaa fupi ni /i/, /e/, /u/, /o/, /a/, /ɪ/, /ɔ/, /ɛ/, /ʊ/ na /ɑ/. Vokali za wakaa refu ni /i:/, /e:/, /u:/, /o:/, /a:/, /ɪː/, /ɔ:/, /ɛ:/, /ʊ:/ na /ɑ:/. Sifa ya wakaa wa vokali ni sifa bainifu katika Kikeiyo kwa sababu huweza kutofautisha maana za maneno. Neno [*ŋget*] kwa mfano, lina maana mbili tofauti kutegemea wakaa wa vokali /e/.

Linapotamkwa kwa wakaa fupi [*ŋget*] lina maana ya “choka”. Vokali /e/ inaporefushwa kuwa [*ŋge:t*] maana inabadilika kuwa “amka”. Jedwali lifuatalo linaonyesha vokali za Kikeiyo na jinsi zinavyotokea katika maneno.

**Jedwali 1: Utambulisho wa Vokali za Kikeiyo**

| **Vokali** | **Othografia** | **Uwakilishi wa kifonetiki** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| i | i | [lit] | noa |
| i: | ii | [biit] | nyunyiza |
| e | e | [tep] | kaa |
| e: | ee | [keer] | ona |
| u | u | [čut] | ingia |
| u: | uu | [kuut] | puliza |
| o | o | [čor] | iba |
| o: | oo | [poor] | kongoa |
| a | a | [tar] | maliza |
| a: | aa | [myaač] | baya |
| ɪ | i̲ | [ɲɪt] | sinya |
| ɪ: | ii | [sɪɪt] | sugua |
| ʊ | u | [tʊč] | funika |
| ʊ: | uu | [mʊʊt] | tano |
| ɛ | e | [ŋɡɛt] | choka |
| ɛ: | ee | [muɡɛɛt] | kifuniko |
| ɔ | o | [pɔl] | piga kelele |
| ɔ: | oo | [jɔɔs] | zee |
| ɑ | a | [čɑm] | penda |
| ɑ: | aa | [tyɑɑŋɡik] | wanyama |

Vokali za Kikeiyo zinaweza kuainishwa kwa misingi ya utaratibu wa mwinuko wa ulimi na mlalo wa ulimi. Kutegemea mwinuko wa ulimi, kuna vokali za juu, vokali za kati-juu, vokali za kati-chini na vokali za chini. Kutegemea mlalo wa ulimi, kuna vokali za mbele, vokali za katikati na vokali za nyuma. Mchoro ufuatao unaonyesha vokali za Kikeiyo kutegemea mwinuko na mlalo wa ulimi;




Lifuatalo ni jedwali la sifa bainifu za vokali za Kikeiyo. Sifa hizi zitatusaidia katika kuchanganua toni za Kikeiyo. Sifa za vokali mbalimbali huathiri toni ya vokali.

**Jedwali 2: Sifa Bainifu za Vokali za Kikeiyo**

| Sauti / Sifa | i | ɪ | e | ɛ | o | ɔ | a | ɑ | u | ʊ |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usilabi | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + |
| Juu | + | + | - | - | - | - | - | - | + | + |
| Nyuma | - | - | - | - | + | + | + | + | + | + |
| Chini | - | - | - | - | - | + | + | + | - | - |
| Mviringo | - | - | - | - | + | + | - | + | + | + |
| Kaze | + | - | + | - | + | - | - | - | + | - |

Kiswahili sanifu tofauti na Kikeiyo kina vokali tano. Vokali hizi ni /i, ɛ, u, ɔ, a/. Vokali za Kiswahili hutokea mwanzo, katikati na mwisho wa silabi. Hii ni sawa na vokali za Kikeiyo. Vokali za Kiswahili ni za wakaa fupi. Vokali za wakaa ndefu hutukia mwishoni mwa neno kibainifu japo kuna maneno machache mno yanayotumia sifa ya wakaa kutofautisha maana zao.

### 2.2.2 Irabu-unganifu za Kikeiyo

Irabu-unganifu huundwa kwa muungano wa vokali mbili ambazo wakati wa utamkaji hutamkwa kama sauti moja, Massamba (2004). Kikeiyo, kwa mujibu wa Chelimo na Randich (2014), kina irabu-unganifu kumi ambazo ni [ai, ei, oi, ui, au, eu, ou, ia, ua, ao]. Hata hivyo, katika utafiti wetu tunatambua aina saba za irabu-unganifu. [ua] na [ia] hatutazizingatia kama irabu-unganifu bali tutazishughulikia katika uundaji wa nusu vokali. Utafiti wetu pia unapinga kuwepo kwa irabu-unganifu [ou] katika Kikeiyo.

Irabu-unganifu [ai] inapatikana katika maneno kama vile:

(5 a) [*ainet*] "mtoni"
(5 b) [*kaigai*] "afadhali"

Irabu-unganifu [ei] inadhihirika katika maneno kama vile:

(6 a) [*mwei*] "toroka"
(6 b) [*čamgei*] "hujambo"

Irabu-unganifu [oi] inapatikana katika maneno kama vile:

(7 a) [*koita*] "jiwe"
(7 b) [*kongoi*] "asante"

Irabu-unganifu [ui] inapatikana katika maneno kama vile:

(8 a) [*muito*] "ngozi"
(8 b) [*tui*] "giza"

Irabu-unganifu [au] inadhihirika katika maneno kama vile:

(9 a) [*baunatet*] "uongozi"

(9 b) [*makaut*] "kiboko"

Irabu-unganifu [eu] inapatikana katika maneno kama vile:

(10 a) [*eut*] "mkono"

(10 b) [*mweu*] "toroka"

Irabu-unganifu [ao] inapatikana katika maneno kama vile;

(11 a) [*kaotik*] "jasho"

(11 b) [*mao*] "kiangazi"

Irabu-unganifu za Kikeiyo ni zile za kufungia, Chelimo na Randich (2014). Irabu-unganifu zinazofungia ni zile zinazohusisha kuinuka kwa ulimi kutoka chini kuelekea juu na hivyo, vokali za chini kuelekea vokali za juu. Irabu-unganifu hizi katika Kikeiyo ni za aina mbili kwa mujibu wa Chelimo na Randich (2014). Kwanza, ni irabu-unganifu za kufungia zinazohusisha vokali za chini kuelekea vokali za juu mbele nazo ni; [ai], [ei], [oi] na [ui]. Aina ya pili ni irabu-unganifu za kufungia zinazohusisha vokali za chini kuelekea vokali za juu nyuma nazo ni; [au] na [eu]. Tunaainisha [ao] katika aina ya pili kwa sababu vokali /o/ ni ya kati nyuma na hivyo, ipo juu ya vokali /a/.

**2.2.3 Konsonanti za Kikeiyo**

Konsonanti, kwa mujibu wa Massamba (2004), ni sauti ambazo wakati wa utamkaji mkondohewa huzuiliwa kwa kiasi kikubwa au kiasi kidogo. Kikeiyo, kwa mujibu wa Chelimo na Randich (2014), kina konsonanti kumi na sita pamoja na nusu vokali mbili. Konsonanti hizi ni; /p (b), t (d), č (y), k (*g*), l, m, n, ɲ, ŋ, r, s, ʃ/. Nusu vokali nazo ni; /j/ na /w/. Katika utafiti wetu, tunaongeza sauti /β/ na /ɣ/ na kuondoa /y/ ambayo haipo katika Kikeiyo. Jumla ya konsonanti za Kikeiyo pamoja na nusu vokali

hivyo basi, ni kumi na tisa. Tumeainisha konsonanti za Kikeiyo ifuatavyo kwa kuzingatia namna ya kuzitamka;

Vipasuo: /p/, /b/, /t/, /d/, /k/ /*g*/
Vikwamizwa: /s/, /β/, /ɣ/ /ʃ/
Kizuiwa-kwamizwa: /č/
Likwidi: /l/, /r/
Nasali: /m/, /n/, /ɲ/, /ŋ/
Nusu vokali: /w/, /j/

Chelimo na Randich (2014), wanatambua kuwa katika Kikeiyo, sifa ya mghuno haitumiki kibainifu. Hii ndio maana konsonanti /p/ na /k/ zina alofoni ambazo hutokea kimpishano huru. Alofoni za [p] ni /p/, /b/ na /β/. [***b****e:ndo*], [***p****e:ndo*] na [***β****e:ndo*] ni maneno yanayorejelea nyama. Maana ya neno haibadiliki japo sauti tofauti zinatumika. Alofoni za [k] ni /k/, /*g*/ na /ɣ/. [***k****u:r*], [*gu:r*] na [***ɣ****u:r*] ni maneno yanayorejelea kitenzi ita. Maana ya maneno haya hayabadiliki japo konsonanti tofauti zinatumika.

Kikeiyo pia kina konsonanti nazalishi ambazo ni /mb/, /ny/, /nd/ na /ŋ*g*/, Chelimo na Randich (2014). Konsonanti nazalishi kwa mujibu wa Mgullu (1999), ni konsonanti zinazochukuliwa kama sauti moja zinapotamkwa pamoja. Konsonanti nazalishi huungana katika mazingira mahususi yanayohusisha fonimu ya kwanza kuwa nasali inapofuatwa na kipasuo. Sauti hizi hutokea mwanzoni mwa silabi kama katika [*ko$****nd****a*] "jicho", [*me$****nyo***] "nyumba ya wavulana waliotahiriwa", [***ŋ****go$ryet*] "nguo" na [*se$****mb****er*] "palilia".

Lifuatalo ni jedwali la uwakilishaji wa IPA na othografia ya konsonanti za Kikeiyo na maneno zinapojitokeza:

**Jedwali 3: Utambulisho wa Konsonanti za Kikeiyo**

| IPA | Othografia | Uwakilishi wa kifonetiki | Maana |
|---|---|---|---|
| /p/→[p], [b], [β] | che**p**to<br>**b**oiyot | [če:**p**to]<br>[**β**oijot] | msichana<br>mzee |
| /t/ | **t**eta | [te:ta] | ng'ombe |
| /d/ | kel**d**o | [ke:ldo] | mguu |
| /k/→ [*g*], [k], [ɣ] | **k**atit<br>la**g**ok | [ka:tit]<br>[laɣo:k] | shingo<br>watoto |
| /s/ | **s**agarik | [sa*g*ari:k] | masagari |
| /ʃ/ | **sh**ool | [ʃo:l] | rusha |
| /č/ | **ch**uguiyet | [čuɣuije:t] | mbwa |
| /l/ | i**l**at | [i:lat] | radi |
| /r/ | **r**i**r**ek | [ri:rek] | kilio |
| /m/ | **m**oet | [moe:t] | tumbo |
| /n/ | **n**wach | [nwač] | fupi |
| /ŋ/ | **ng'**ororiet | [ŋ*g*ororiet] | kondoo |
| /ɲ/ | **ny**alilda | [ɲalilda] | shida |
| /j/ | **y**osindo | [josindo] | uzee |
| /w/ | **w**erit | [weri:t] | mtoto wa kiume |
| /mb/ | **mb**aret | [mbare:t] | shamba |
| /nd/ | **nd**aret | [ndare:t] | nyoka |
| /ŋ*g*/ | **ng**oryet | [ŋ*g*orye:t] | nguo |
| /ny/ | me**nj**o | [me:nyo] | nyumba ya wavulana waliotahiriwa |

Kikeiyo kina silabi funge KVK na KV:K inayopelekea konsonanti na nusu vokali kuweza kuchukua nafasi za kwanza na mwisho katika silabi. Katika nomino [*kito:g*] "kitanda" kwa mfano, kuna silabi {to:*g*} yenye mwanzo silabi na koda ambazo ni konsonanti /t/ na /*g*/ mtawalia.

Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha konsonanti za Kikeiyo na sifa zinazobainisha konsonanti hizo:

**Jedwali 4: Sifa Bainifu za Konsonati za Kikeiyo**

| **Sauti** / **Sifa** | p | b | β | m | t | d | n | k | *g* | ɣ | ɳ | S | ʃ | č | l | r | ŋ | w | j |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usilabi | - | - | - | + | - | - | + | - | - | - | + | - | - | - | - | - | + | - | - |
| Konsonanti | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + | + | - | - |
| Sonoranti | - | - | - | + | - | - | + | - | - | - | + | - | - | - | + | + | + | + | + |
| Ghuna | - | + | - | + | - | - | + | - | + | - | + | - | - | - | - | - | + | - | - |
| Kontinuanti | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | + | + | - | - | - | - | - | - |
| Nasali | - | - | - | + | - | - | + | - | - | - | + | - | - | - | - | - | + | - | - |
| Stridenti | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | + | + | + | - | - | - | - | - |
| Kilainisho | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | + | - | - | - | - |
| Msambao | - | - | + | - | - | - | - | - | - | - | - | - | + | - | - | - | - | - | - |
| Kizuiwa-kwamizwa | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | + | - | - | - | - | - |
| Midomo | + | + | + | + | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | + | - |
| Mviringo | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | + | - | + | + |
| Korona | - | - | - | - | + | + | + | - | - | - | - | + | + | + | + | + | + | - | - |
| Anteria | + | + | + | + | + | + | + | - | - | - | - | + | - | - | + | + | - | - | - |
| Juu | - | - | - | - | - | - | - | + | + | + | + | - | + | + | - | - | + | + | + |
| Nyuma | - | - | - | - | - | - | - | + | + | + | + | - | - | - | - | - | - | + | - |
| Chini | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |

### 2.2.4 Uundaji wa Nusu Vokali za Kikeiyo

Kikeiyo kama tulivyokwisha kuonyesha kina nusu vokali mbili ambazo ni /w/ na /j/. Nusu vokali hizi huundwa katika mazingira mahususi kama ifuatavyo:

**Uundaji wa /w/**

Nusu vokali ya midomo /w/, huundwa katika mazingira ya vokali za nyuma juu /u/ na /ʊ/ zinapofuatwa na vokali za chini /a/ na /ɑ/ kama inavyoelezwa kwenye mfanyiko ufuatao:

u ⟶ w/__a

Mifano ya mfanyiko huu:

(12 a) /ku+a+nit/ ⟶ [kwanit] "baba"

(12 b) /ku+a+ɲ/ ⟶ [kwaɲ] "songa ugali"

(12 c) /ku+a+am/ ⟶ [kwa:m] "nilikula"

**Uundaji wa /j/**

Nusu vokali ya kaakaa /j/ huundwa katika mazingira ya vokali za juu mbele /i/ na /ɪ/zinapofuatwa na vokali za chini /a/ na /ɑ/ kama katika mfanyiko ufuatao:

i ⟶ j/ __ a

Mifano ya mfanyiko huu ni:

(13 a) /ki+a+wendi/ ⟶ [kjawendi] "nilienda"

(13 b) /ki+a+ɡuur/ ⟶ [kjaɡuur] "nilimuita"

(13 c) /ki+a+laɲ/ ⟶ [kjalaɲ] "nilipanda"

Kiswahili, tofauti na Kikeiyo kina konsonanti halisi ishirini na tano na nusu vokali mbili, Iribemwangi (2010). Konsonanti hizi ni /p, b, t, d, k, ɡ, h, f, v, s, ʃ, z, x, č, y, l, r, ɣ, θ, ð, ɱ, ɲ, m, n, ŋ /. Pamoja na konsonanti hizi halisi, kuna nusu vokali mbili /w,

j/. Kiswahili pia kama Kikeiyo kina konsonanti nazalishi ambazo ni /mb, nd, nz, nj, nt, nč/, Mgullu (1999).

## 2.3 Fonolojia Arudhi ya Kikeiyo

Kikeiyo kina sifa za kiarudhi za silabi, toni, mkazo, wakaa na kiimbo miongoni mwa sifa nyingine. Sifa tatu za mkazo, toni na silabi ndizo zinashughulikiwa katika utafiti huu.

### 2.3.1 Silabi za Kikeiyo

Sifa za kiarudhi hudhihirika katika silabi. Utafiti huu ulihusisha silabi kama sifa ya kiarudhi. Dhana ya silabi imeelezwa na wataalamu kama vile Hyman (1975), Lass (1984) na Fromkin n.w (2003), kama kipashio cha kifonolojia kinachowakilisha umbo la kimatamshi ambapo sauti moja au nyingi zinatamkwa kama fungu moja. Silabi inajengwa kwa viambajengo viwili vikuu ambavyo ni mwanzo silabi na upeo silabi. Upeo silabi unajengwa kwa kiini cha silabi na koda. Katika utafiti huu, tulichunguza miundo ya silabi ya Kikeiyo.

Kenstowicz na Kisserberth (1979), wanatambua kwamba katika uwakilishi wa kifonetiki sauti za lugha hupangwa katika vipashio vikubwa kuliko vipandesauti na silabi ni mojawapo ya vipashio hivyo. Silabi ni umbo la kimatamshi ambapo sauti moja au zaidi hutamkwa kwa mara moja, Hyman (1975). Kila lugha huwa na taratibu za kuunda silabi zake na hivyo, miundo ya silabi ni tofauti katika lugha mbalimbali.


#### 2.3.1.1 Silabi Wazi

Kwa mujibu wa Hyman (1975), Ladefoged (1975) na O’Grady, n.w (1997), silabi wazi haina koda. Kikeiyo kina miundo mbalimbali ya silabi hii.


**Silabi ya KV**

Lugha zote kwa mujibu wa Clements na Keyser (1983), zina aina hii ya silabi na Kikeiyo ni mojawapo ya lugha hizi. Silabi hii ni mojawapo ya silabi pendwa katika Kikeiyo na hutokea mwanzoni, katikati au mwishoni wa neno kama ifuatavyo:

(14 a) [ro:p$**ta**] “mvua”





(14 b) [*ko*$***ro*$***ti:k*]“damu”





**Silabi ya V**

Kikeiyo kina vokali fupi ambazo huweza kusimama kama silabi katika maneno bila ya kuandamana na koda au mwanzo. Silabi hii huweza kutokea mwanzo, katikati au mwisho wa neno kama ifuatavyo:

(15 a) [***i*$***man*] “ukweli”




(15 b) ***[o**$re:t]* “barabara”





**Silabi ya V:**

Silabi hii huundwa kwa vokali moja ya wakaa refu na huweza kutokea mwanzoni na katikati ya neno kama katika:

(16 a) [*bo*$*ro*$***i*$***ndo*]“fursa”.





(16 b) [***i*:$***tit*] “sikio”





**Silabi ya KV:**

Silabi hii huundwa kwa konsonanti moja na vokali moja yenye wakaa refu. Silabi hii huweza kutokea mwanzoni na katikati ya neno kama katika:

(17 a) [***ku:*** *go*] “babu”




(17 b) [*či:*] “mtu”





**Silabi ya KKV**

Silabi hii huundwa kwa konsonanti moja, nusu vokali moja na vokali moja ya wakaa fupi. Silabi hii huweza kutokea mahali popote katika neno kama katika:

(18 a) [***kwo****ndo*]“mke”





(18 b) [*mer****kwe****ti:n*] “mmarakwet





**Silabi ya KKV:**

Silabi hii huundwa kwa konsonanti moja, nusu vokali moja na vokali moja ya wakaa refu. Silabi hii huweza kutokea mahali popote katika neno kama katika:

(19 a) **[*tyo:*$*ndo*]** “mnyama wa pori”.



(19 b) [***rwa:****$nde:t*] “jiwe”





### 2.3.1.2 Silabi Funge

Silabi funge ni silabi zilizo na koda. Silabi hizi huweza kuwa na mwanzo silabi au kukosa kuwa na mwanzo silabi. Kikeiyo kina aina mbalimbali ya silabi funge.


**Silabi ya KVK**

Hii ndio silabi pendwa katika Kikeiyo. Silabi hii huundwa kwa konsonanti moja, vokali moja ya wakaa fupi na konsonanti. Silabi hii hutokea mahali popote katika neno kama katika:

(20 a) [*i:*$***tit***] “sikio”





(20 b) [*met*] “kichwa”





**Silabi ya VK**

Silabi za aina hii huundwa kwa vokali moja fupi na konsonanti. Silabi hii hutokea mwanzoni mwa neno kama katika:

(21 a) [***ur***$*we:t*] “kivuli”





(21 b) [***ar****$te:t*] “mbuzi”





**Silabi ya KV:K**

Silabi hizi huundwa kwa konsonanti moja, vokali moja ya wakaa refu na konsonanti. Silabi hizi hutokea mahali popote katika neno kama katika:

(22 a) [*si*$*gir*$***ye:t***] “punda”





(22 b) [*te*$*g**a:t***]“mwanzi”.





**Silabi ya V:K**

Silabi hizi huundwa kwa vokali moja ya wakaa refu na konsonanti. Silabi hizi hutokea mwanzoni na mwishoni mwa neno kama katika:

(23 a) [*mo**e:t***] “tumbo”





(23 b) [oɳ**a:t**] “jangwa”





**Silabi ya KKVK**

Silabi za aina hii huundwa kwa konsonanti moja, nusu vokali moja, vokali ya wakaa fupi na konsonanti. Huweza kutokea mahali popote katika neno kama:

(24 a) [*ra$**bwon**$ik***]** “viazi vitamu”





(24 b) [ŋweɲ] “sakafu”





**Silabi ya KKV:K**

Silabi hii huundwa kwa konsonanti moja, nusu vokali moja, vokali moja ya wakaa refu na konsonanti. Huweza kutokea mahali popote katika neno kama katika:

(25 a) [*ro*$***rja:t*]** “fahali”




(25 b) [*kipsoi**jwe:t***] “jogoo”




Silabi zinaweza kuwa nyepesi au nzito. Kwa kurejelea maelezo ya wataalamu kama vile Lass (1984), Clements na Keyser (1983), Goldsmith (1990) na Hyman (2003), silabi nzito ni silabi yenye uchangamano kwa sababu, upeo wa silabi huwa na tawi linalogawika. Hyman (1975), anatambua kuwa lugha zilizo na silabi nzito na silabi nyepesi huwa na ukinzani wa sifa ya wakaa. Kuna ukinzani kati ya KV na KV:. Kiuzani, KV: inafanana na KVK. Kikeiyo kimedhihihirisha uwepo wa vokali za silabi nzito na silabi nyepesi.

Kiswahili sanifu kina miundo tofauti ya silabi na zile za Kikeiyo. Kiswahili kina miundo ya silabi ya KV (silabi pendwa) na V. Silabi hizi hupatikana kwa maneno ya kiasilia, Mwaliwa (2014). Miundo mingine ya KVK na VK ni miundo inayotokana na maneno mkopo, Mgullu (1999) na Mwaliwa (2014). Jumla ya silabi msingi katika Kiswahili ni KV, V, KVK na VK. Miundo mingine ya silabi kwa mujibu wa Iribemwangi (2010:53-58), ni KKV yenye kuundwa kwa konsonanti mbili na vokali, KKKV yenye kuundwa kwa konsonanti mbili, nusu vokali na vokali, K yenye kuundwa kwa konsonanti moja, KVV yenye kuundwa kwa konsonanti moja na vokali

refu na KKKV inayoundwa kwa konsonanti tatu na vokali moja na hupatikana katika maneno mkopo. Silabi zote za Kiswahili hivyo basi ni tisa.

### 2.3.2 Mkazo Katika Kikeiyo

Massamba (2012), anafasiri mkazo kama sifa ya kiarudhi inayopelekea silabi moja katika neno kutamkwa kwa nguvu zaidi kuliko silabi nyingine. Kutokana na kutamka silabi moja kwa nguvu zaidi, kwa mujibu wa Hogg na McCully (1987), silabi hiyo inarefusha vokali yake, kidatu kinapandishwa na sauti ya kutamkia inaongezeka. Kama inavyoelezwa na Chomsky na Halle (1968), mkazo ni sehemu ya silabi na hasa vokali inayohusishwa na mkazo huo.

Mahali mkazo unapowekwa katika neno, huathiriwa na masuala ya kiisimu kama vile mipaka ya maneno, kategoria za maneno na mifumo ya kifonolojia, Hyman (1975). Hii inapeleka kuwepo kwa aina mbili za lugha mkazo, Hyman (1975). Kuna lugha zenye mkazo changamani. Lugha hizi huwa na uhuru wa mkazo. Uhuru wa mkazo unatokana na hali kwamba miundo ya silabi huathiri mahali mkazo unawekwa. Lugha inapokuwa na uhuru wa mkazo kwa mujibu wa Garde (1967), haimaanishi kuwa mkazo unaweza kuwekwa mahali popote. Mkazo unapokuwa huru, ina maana kuwa, kutegemea miundo ya kifonolojia ya lugha, mkazo unaweza kubainishwa. Aina ya pili ni lugha zenye mkazo sahili. Lugha hizi huweka mkazo katika silabi mahususi bila kujali miundo yao. Kiswahili, ni mfano wa lugha yenye mkazo sahili inayoweka mkazo katika silabi ya pili kutoka mwisho isipokuwa katika baadhi ya maneno, Mwaliwa (2014).

Lugha zenye mkazo sahili huteua silabi moja tu ambayo huwekewa mkazo. Lugha zenye mkazo changamani kwa upande mwingine, huathiriwa na miundo ya silabi katika kuwekea silabi zake mkazo, O’Grady n.w (1997) na Hyman (2003). Katika


lugha nyingi, mkazo huwekwa kwenye silabi nzito. Iwapo neno halina silabi nzito, kila lugha ina mikakati tofauti ya kuwekea silabi hizo nyepesi mkazo. Uzani wa silabi ni kipashio muhimu cha kifonolojia kinachoathiri namna mkazo huwekewa maneno katika lugha nyingi.

Katika 2.3.1, tumeelezea miundo ya silabi za Kikeiyo. Kutokana na hali kwamba uzani wa silabi huathiri mahali mkazo unawekwa, tunaweza kubainisha silabi nzito na nyepesi na kuona namna zinavyoathiri mahali mkazo unawekwa.


#### 2.3.2.1 Mkazo Katika Maneno Yenye Silabi Moja

Katika maneno yanayoundwa kwa silabi moja, mkazo huangukia vokali katika neno hilo, (Goldsmith 1990). Kikeiyo kina maneno mengi yanayoundwa kwa silabi moja. Silabi hizi huweza kuwa nzito au nyepesi. Mkazo katika maneno haya unakuwa kwenye vokali ya silabi hiyo moja kama katika:

(26 a) [*met*] “kichwa”




(26 b) [*či:*] “mtu”





Neno [*met*] lina muundo wa silabi KVK na [*či:*] lina muundo wa KV:. Mkazo katika maneno haya upo kwenye vokali ambayo inajengewa futi.

### 2.3.2.2 Mkazo Katika Maneno Yenye Silabi Mbili


Maneno yanayoundwa kwa silabi mbili huwekea silabi zao mkazo kutegemea miundo ya silabi hizo. Maneno mengi ya Kikeiyo yanaundwa kwa silabi mbili. Silabi hizi hata hivyo, zina uzani tofautitofauti kama ifuatavyo:

(27a) [*be*$*tu:t*]"siku"




Neno hili linaundwa kwa silabi mbili ambazo ni silabi nyepesi {be} yenye muundo wa KV na silabi nzito {tut} yenye muundo wa KVK. Kama inavyopendekezwa kwenye nadharia ya FVH, kila silabi nzito katika neno inapokea mkazo. Kwa hivyo, mkazo katika neno hili upo katika silabi ya mwisho ambayo ni silabi nzito. Futi ya kimetrika ni ya kulia.

(27 b) [*ker*$*čo:t*] "dawa"





Neno hili linaundwa kwa silabi mbili nzito. Silabi ya kwanza ni {ker} yenye muundo wa KVK na silabi ya pili ni {čo:t} yenye muundo wa KV:K. Kama inavyopendekezwa katika nadharia ya FM, kila silabi nzito inapaswa kuwekewa mkazo. Mkazo msingi katika neno inapaswa kuwa moja kama inavyoelezwa na Verma na Krishnaswamy (1989). Inapotokea kuna silabi nzito zaidi ya moja, mkazo utawekwa kwa namna tofauti kutegemea lugha. Kikeiyo hutumia mkazo kubainisha

idadi ya nomino. Katika mfano (27b), mkazo unawekwa katika silabi ya mwisho. Futi ya kimetrika ni ya kulia.

### 2.3.2.3 Mkazo Katika Maneno Yenye Silabi Nyingi


Katika kikundi hiki, tunapata maneno yanayoundwa kwa zaidi ya silabi mbili. Silabi hizo zina miundo tofautitofauti. Mkazo utawekwa katika silabi mahususi kutegemea miundo yao kama ifuatavyo:

(28 a) [*i*$*ŋgor*$*ye:t*] "nguo"




Neno hili lina silabi tatu. Silabi ya kwanza {i} ni ya vokali fupi, silabi ya pili {ŋgor} ni ya muundo wa KVK na silabi ya mwisho {e:t} ina muundo wa V:K. Silabi ya pili na ya mwisho ni silabi nzito na kama katika (27 b), mkazo unawekwa katika silabi ya mwisho yenye kiambishi cha idadi. Futi ya kimetrika ni ya kulia.


(28 b) [*so*$*noi*$*ya:t*] "shanga"




Neno hili lina silabi tatu zenye miundo tofauti. Silabi ya kwanza ni {so} yenye muundo wa KV. Silabi ya pili ni {noi} yenye muundo wa KV ambapo V ni irabu-unganifu. Silabi ya tatu ni {ya:t} yenye muundo wa KV:K. Silabi nzito katika neno hili ni mbili, silabi ya pili na ya tatu. Kama tulivyokwisha kuonyesha awali, maneno

yenye silabi nzito mbili huwekea mkazo katika silabi nzito ya mwisho. Mkazo hivyo basi, upo katika silabi ya mwisho. Futi ya kimetrika ni ya kulia.

(28 c) [*kul$gul$da*]“makwapa”




Neno hili lina silabi tatu. Silabi ya kwanza ni {kul} yenye muundo wa KVK. Silabi ya pili ni {gul} pia yenye muundo wa KVK. Silabi ya tatu ni {da} yenye muundo wa KV. Silabi nzito ni za kwanza mbili. Mkazo unawekwa katika silabi nzito ya pili.Futi ya kimetrika ni ya kulia. Silabi ya tatu ni silabi baki kwa sababu inakuja baada ya silabi inayowekewa mkazo na hivyo, haihusishwi na futi ya kimetrika.

Kuna kanuni zinazothibiti namna mkazo unavyowekwa katika neno, Goldsmith (1990). Kwanza, ni mkazo unaowekwa katika sehemu mahususi kama katika Kiswahili. Pili, kuna mkazo unaowekwa kutegemea muundo wa kimofolojia wa neno na mwisho, ni mkazo unaowekwa kutegemea muundo wa silabi. Kutokana na kanuni hizi, tunahitimisha kuwa Kikeiyo ni lugha inayotegemea muundo wa silabi katika kuwekea maneno yake mkazo. Kikeiyo hivyo basi, kulingana na uainishaji wa Hyman (1975), ni lugha yenye mkazo changamani inayoweka mkazo kutegemea miundo ya silabi.

Mkazo huwa na majukumu ya kifonolojia katika lugha, Massamba (2012). Kwa mfano, katika Kiingereza, mkazo hutumiwa kubainisha kategoria za maneno zinazofanana. Katika Kikeiyo, imebainika kupitia mifano yetu kuwa mkazo huwa na jukumu la kifonolojia la kuonyesha idadi ya nomino.

Kiswahili, kama kinavyoelezwa na Mgullu (1999), na Massamba (2011), ni lugha inayowekea maneno yake mkazo katika silabi ya pili kutoka mwisho isipokuwa katika baadhi ya maneno, Mwaliwa (2014). Kiswahili hivyo basi, kulingana na uainishaji wa Hyman (1975), ni lugha yenye mkazo sahili wa mahali mahususi.

### 2.3.3 Toni Katika Kikeiyo

Toni ni kipashio cha kiisimu ambacho hutumia kidatu katika kutofautisha maana za maneno, Yip (2002). Toni hivyo basi, huwa na jukumu la kuleta tofauti za kimaana katika baadhi ya lugha ambazo hujulikana kama lugha toni, Nathan (2008). Lugha toni ni lugha ambazo hutumia kidatu kubainisha maana za maneno na uamilifu wa kisarufi, Yip (2002). Kikeiyo ni lugha toni kwa sababu, kinatumia sifa ya toni kutofautisha maana za baadhi ya maneno. Kwa mfano, neno [*moet*] lina maana tofauti kutegemea namna kidatu kinavyotumika. Neno hili lina maana ya "tumbo" linapotamkwa kwa toni chini juu [*mòét*]. Maana ya pili ni "kidonda" linapotamkwa kwa toni chini chini [*mòèt*].

Cherono n.w (2015), wanaainisha aina tatu za toni msingi katika Kikeiyo ambazo ni toni juu[4], toni chini[5] na toni kati[6]. Pamoja na toni hizi za kimsingi, kuna toni za mpandushuko ambazo ni toni panda[7] na toni shuka[8]. Toni za mpandashuko zinapatwa kutokana na kuunganisha toni za kawaida, Massamba (2004).

#### 2.3.3.1 Toni Katika Nomino za Kikeiyo

Kikeiyo kama tulivyokwisha kueleza katika 1.1.1 kina maumbo mawili ya nomino zake. Maumbo haya ni maumbo msingi yanayorejelea nomino kwa ujumla na

---

[4]Toni juu- toni inayodhihirishwa na kidatu cha juu
[5]Toni chini- toni toni inayodhihirishwa na kidatu cha chini
[6]Toni kati- toni inayodhihirishwa na kidatu cha kati
[7]Toni panda- toni inayodhihirishwa na kidatu cha mpandashuko kuanzia chini kwenda juu
[8]Toni shuka- toni inayodhihirishwa na kidatu cha mpandashuko kuanzia juu kwenda chini

maumbo ya upili yanayorejelea nomino zinazofahamika. Toni hudhihirika tofauti katika nomino za maumbo haya.

Tunatumia ishara zifuatazo kuonyesha aina mbalimbali za toni katika Kikeiyo;

Toni kati (K) - a

Toni chini (C) - à

Toni juu (J) – á

Toni panda (P) -ǎ

Toni shuka (S) – â

**Jedwali 5: Uwakilishi wa Toni Katika Nomino za Umoja**

| **Nomino za kimsingi** | **Nomino za upili** |
|---|---|
| [sot] “kibuyu” | [sòtéét] |
| [met] “kichwa” | [mètít] |
| [moì] “ndama” | [moítà] |
| [čorwà] “rafiki” | [čòrwéét] |
| [kaínà] “jina” | [kàínéét] |
| [kééčíír] “kondoo” | [kèčirìét] |

Idadi ya toni katika neno hutegemea idadi ya silabi katika neno hilo. Toni hupachikwa kwenye VVT na vipashio hivi ni vokali. Aina mbalimbali za vokali huwa na toni za aina tofauti, Clark na Yallop (1995), ambao wanasema vokali za juu /i/ na /u/ huwa za toni juu, vokali ya chini /a/ huwa ya toni chini na vokali za kati /e/ na /o/ ni za toni kati. Katika Kikeiyo, hali hii hudhihirika kama inavyojadiliwa na Chelimo n.w (2015). Japo, kutegemea miundo ya silabi za maneno, vokali mbalimbali zinaweza kuwa za toni tofauti. Katika jedwali la tano, vokali za juu kama vile /i/ katika [*kaína*] “jina” inatamkwa kwa toni juu. Vokali /a/ katika [*čorwà*] “rafiki”inatamkwa kwa toni chini. Vokali /o/ katika [*moì*] “ndama” inatamkwa kwa toni kati.

Nomino za kimsingi katika jedwali la tano zinadhihirisha toni za aina mbalimbali. Nomino zinazoundwa kwa silabi moja, hutamkwa kwa toni kati kama katika [*sot*] “kibuyu”na [*met*]. Vokali /o/ na /e/ zinatamkwa kwa toni kati. Panapokuwa na silabi ya pili katika nomino za kimsingi, vokali katika silabi hiyo hutamkwa kwa toni chini kama katika [*čorwà*] na [*moì*].

Katika maumbo ya upili, kuna viambishi vya idadi vinavyoongezwa. Toni katika nomino za kimsingi huathiri toni za viambishi vinavyoongezewa nomino hizo katika maumbo ya upili na katika wingi, Chelimo n.w (2015). Vokali /o/ katika nomino [*sot*] “kibuyu” kwa mfano, ni ya toni kati. Katika umbo la upili [*sòtéét*], toni kati ya mzizi ambao pia ni umbo la kimsingi inabadilika na kuwa toni chini kama ifuatavyo;

K ⟶ C/ umbo la upili

Maumbo ya upili yana silabi mbili na zaidi. Katika nomino zenye silabi mbili, silabi ya kwanza hutamkwa kwa toni chini na ya pili hutamkwa kwa toni juu. Muundo wa toni katika nomino za silabi mbili kwa hivyo ni, chini juu (CJ) kama katika [*mètít*] “kichwa”. Nomino zinapokuwa na silabi tatu, silabi ya kwanza inatamkwa kwa toni chini, silabi ya pili kwa toni kati na silabi ya tatu kwa toni juu. Muundo wa toni hivyo basi ni, chini kati juu (CKJ). Kanuni ya usilimisho ni kwamba, silabi ya kwanza ya umbo msingi inayotamkwa kwa toni kati hubadilika katika umbo la upili na kutamkwa kwa toni chini;

(29 a) moì ⟶ mòítà

K ⟶ C ╱ umbo la upili

o ⟶ ò ╱ umbo la upili

nayo silabi ya pili inayotamkwa kwa toni chini inabadilika na kutamkwa kwa toni juu;

C ⟶ J ╱ C ___

ì ⟶ í ╱ ò___

(29 b) čorwà ⟶ čòrwéét

o ⟶ ò/ umbo msingi

à ⟶ é/ò ——

Katika nomino za upili za silabi tatu, silabi ya kwanza inatamkwa kwa toni chini, silabi ya pili kwa toni kati na silabi ya tatu kwa toni juu.Muundo wa toni ni toni chini kati juu (CKJ) kama katika [*kèčiríét*] "kondoo" na [*sìgiryéét*] "punda".

Maneno yenye kuundwa kwa irabu-unganifu yana toni za mpandashuko. Neno [*mòíta*] "ndama" kwa mfano, linaundwa kwa irabu-unganifu [oi]. Irabu-unganifu hii ni ya toni panda. Neno [*baúnatéét*] "uongozi" lina irabu-unganifu [au] inayotamkwa kwa toni panda. Katika maumbo haya ya upili, inaonekana pia kuwa sifa za vokali mbalimbali zinazingatiwa wakati wa utamkaji. Vokali za juu kwa mfano, zinatamkwa kwa toni juu kama katika neno [*mètít*] "kichwa', vokali /i/ ni ya toni juu. Hata hivyo, baadhi ya sifa hizi zinakiukwa. Kwa mfano, vokali /o/ inayotamkwa kwa toni kati inapokuwa katika silabi ya kwanza ya neno lenye silabi mbili, inatamkwa kwa toni chini kama inavyodhihirika katika neno [*sòt$éét*] "kibuyu".

Vokali zinapokuwa za wakaa refu, vokali hizo huwakilishwa kama vokali mbili za wakaa fupi. Vokali hizi hupokea toni juu kama katika [*kàínéét*] "jina"na [*čòrwéét*] "rafiki". Katika nomino hizi, vokali /e:/ inawakilishwa kama /ee/. Vokali hii ni ya kati na kawaida inapaswa kuwa ya toni kati. Sifa ya vokali hii inakiukwa na kuwa ya toni juu kwa sababu inarefushwa na kuwa nzito. Silabi nzito hutamkwa kwa tonijuu, Chelimo n.w (2015).

**Jedwali 6: Uwakilishi wa Toni Katika Nomino za Wingi**

| Nomino | Nomino za kimsingi | Nomino za Upili |
|---|---|---|
| [sòtéét] “kibuyu” | [sotóón] | [sotóóník] |
| [kèčiryèt] “kondoo” | [kèčíír] | [kèčíírék] |
| [čìtó] “mtu” | [bííč] | [bíík] |
| [čèptó] “msichana” | [tìbíín] | [tìbíík] |
| [kètít] “mti” | [kètíín] | [kètíík] |
| [kàtéét] “sindano” | [kàtoí] | [kàtóók] |

Viambishi vya wingi vinapoongezewa nomino, toni hubadilika. Nomino za kimsingi huchukua viambishi {-in}, {-on} na {-oi} katika wingi. Viambishi hivi hubeba toni za aina tofauti, Chelimo n.w (2015). Viambishi vya wingi vya nomino za upili ni {-ik},{-ek} na {-ok} vinavyobeba toni tofauti. Kiambishi {-ik} ni cha toni juu, kiambishi {-ek} ni cha toni kati na {-ok} ni cha toni chini. Viambishi hivi hata hivyo, huweza kuchukua toni tofauti kutegemea miundo ya silabi. Kiambishi {on} kwa mfano, ni cha toni kati lakini katika [*sotóón*] “vibuyu” kiambishi hiki kinachukua toni juu kwa sababu vokali /o/ inarefushwa na hivyo kuifanya silabi kuwa nzito na kuwa ya toni juu.

Katika nomino kwenye jedwali la sita, inaonekana kuwa vokali za kati zenye toni kati katika silabi ya kwanza zinapofuatwa na vokali za juu katika silabi jirani hushusha toni kati kuwa toni chini kama katika;

(30)[*kètíín*]“miti”

K → C / ___ J

e → è / ___ í

Katika nomino hii, vokali /e/ ni ya kati na hivyo, ya toni kati lakini inafuatwa na vokali /i/ ambayo ni ya juu na hivyo ya toni juu. Vokali /i/ ya juu inasababisha vokali /e/ ya kati kuwa ya toni chini.

Nomino za wingi zenye kuundwa kwa silabi mbili katika mifano kwenye jedwali la sita, zina miundo ya toni chini juu (CJ). Silabi za kwanza ni za toni chini na silabi za pili ni za toni juu kama katika kwenye nomino [*kètíík*] "miti" na [*kàtóók*] "sindano".

Katika nomino zenye silabi tatu, silabi ya kwanza ni ya toni chini, silabi ya pili ya toni kati na silabi ya tatu ya toni juu. Katika maneno [*tùmaéék*] "majani" na [*mùreníík*] "vijana wa kiume", toni zina mfuatano wa chini kati juu (CKJ).

**2.3.3.2 Majukumu ya Toni Katika Kikeiyo**

Toni hutekeleza majukumu mbalimbali katika lugha, Verma na Krishnaswamy (1989), Fox (2000) na Yip (2002). Toni ina majukumu ya kileksika na majukumu ya kisarufi. Jukumu la kileksika la toni ni kutofautisha maana za maneno. Toni mbalimbali huweza kujibainisha kileksika katika mazingira fulani maalumu kifonolojia, Hyman (1975:213). Umbo moja la neno linaweza kuzaa maana tofauti. Katika Kikeiyo kwa mfano, maneno [*pet*], [*moet*], [*sogeek*] na [*ŋget*] yana maana tofautitofauti. Tofauti ya maana ya maneno haya inajitokeza katika matumizi tofauti ya toni.

(31 a) [*pèt*]"pasua" C  (31 b) na [*pét*]"potea" J.

| | | |
|---|---|---|
| Rusu ya fonimu | P e t | p e t |
| Rusu ya KV | K V K | K V K |
| Rusu ya toni | C | J |

(32 a) [*mòét*]“kidonda” CJ (32 b) [*mòèt*]“tumbo” C (32c)[*móét*]“msikataze” J.

| | (32 a) | (32 b) | (32 c) |
|---|---|---|---|
| Rusu ya fonimu | m o e t | m o e t | m o e t |
| Rusu ya KV | K V V K | K V VK | K V VK |
| Rusu ya toni | C J | C C | J J |

(33 a)[*ŋgét*]“choka” J (33 b)[*ŋgèt*]“katika” C.

| | (33 a) | (33 b) |
|---|---|---|
| Rusu ya fonimu | ŋ*g* e t | ŋ*g* e t |
| Rusu ya KV | K V K | K V K |
| Rusu ya toni | J | C |

Katika jozi hizi, maneno yanafanana kwa misingi ya konsonanti na vokali zinazotumika kuyaundia. Tofauti ya maneno haya inatokana na toni zinazotumika kuyatamkia.

Jukumu la kisarufi la toni ni kutofautisha kategoria za maneno katika lugha. Katika Kikeiyo, toni inatumika kutofautisha maneno katika kategoria mbalimbali kama vile nomino, vitenzi na vivumishi. Kuna maneno ya kategoria mbalimbali yanayofanana na huhitaji toni kubainisha kategoria ya maneno hayo. Maneno yafuatayo yanafanana kwa misingi ya konsonanti na vokali. Tofauti ya maneno haya ni katika toni.

(34 a) [*sír*] “andika”- kitenzi (34 b) [*sìr*] “chunusi”- nomino

(35 a) [*páì*] “lisha”- kitenzi (35 b) [*pàí*] “mahindi”- nomino

(36 a) [*méét*] “usikataze”- kitenzi (36 b) [*mèèt*] “kifo” – nomino

(37 a) [*úí*] “enda” – kitenzi (37 b) [*úì*] “ngumu”- kivumishi

(37 c) [*ùì*] “mahali”- kielezi

(38 a) [*kóì*] “refu” - kivumishi (38 b) [*koì*] “jiwe” – nomino

(39 a) [*sím*] “sherehekea” – kitenzi (39 b) [*sìm*] “uchafu” - kivumishi

Kutokana na mifano hii, ni bayana kuwa Kikeiyo ni lugha inayotumia sifa ya toni kubainisha kategoria za maneno yake. Kiswahili tofauti na Kikeiyo si lugha toni, Massamba (2011).

## 2.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeonyesha sifa za kiarudhi zinazopatikana katika Kikeiyo. tumeona kuwa Kikeiyo kina aina mbalimbali ya silabi wazi na funge. miundo ya silabi hizi huathiri mkazo unapowekwa. Kikeiyo, ni lugha inayotegemea uzani wa silabi katika kuwekea maneno yake mkazo. Mwisho tumebainisha kuwa sifa ya toni ipo katika Kikeiyo. toni ina majukumu mawili ya kubainisha maana za maneno na pia kubainisha maneno katika kategoria mbalimbali. Kuna pia uhusiano kati ya uzani wa silabi na mkazo. Silabi zinazotiliwa mkazo ni za toni juu.

# SURA YA TATU

# FONOLOJIA ARUDHI YA NOMINO MKOPO ZA KIKEIYO

## 3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili, tulielezea fonolojia ya Kikeiyo. Uchanganuzi huo ulihusisha fonolojia vipandesauti na fonolojia arudhi ya Kikeiyo. Uchanganuzi wa fonolojia ya Kikeiyo ndio uliwekea msingi uchanganuzi wa fonolojia arudhi ya nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili unaofanywa katika sura hii.

Kiswahili na Kikeiyo ni lugha zinazotofautiana kiarudhi. Kama tulivyoonyesha katika sura ya pili, Kiswahili na Kikeiyo ni lugha mkazo. Tofauti ni katika namna lugha hizi huwekea maneno yao mkazo. Kikeiyo ni lugha yenye mkazo changamano. Uzani wa silabi huathiri mahali mkazo unapowekwa. Kiswahili nacho kina mkazo sahili. Mkazo huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho isipokuwa katika baadhi ya maneno.

Kikeiyo ni lugha toni inayotumia sifa ya kidatu katika maneno yake kutofautisha maana za maneno. Toni pia inatumika kutofautisha kategoria mbalimbali za maneno. Hii ni tofauti na Kiswahili inayokosa sifa ya toni.

Kwa mujibu wa Kang (2010), lugha inapokopa maneno, lazima maneno hayo yatoholewe ili yaingiliane na miundo ya lugha pokezi. Nomino za Kiswahili zinapoingia katika leksimu ya Kikeiyo, huwa na sifa za kiarudhi za Kiswahili. Nomino hizo hutoholewa ili ziingie katika mifumo ya kiisimu ya Kikeiyo. Zinapotoholewa, nomino hizi hupokea sifa za kiarudhi za Kikeiyo.

## 3.2 Silabi Za Nomino Mkopo za Kikeiyo

Katika 2.3.1, tuliona kuwa Kiswahili kina miundo ya silabi ambayo ni tofauti na zile zinazopatikana katika Kikeiyo. Silabi pendwa katika Kiswahili ni KV. Silabi pendwa katika Kikeiyo ni KVK na KV. Maneno yanayokopwa kutoka Kiswahili sanifu


hutoholewa katika Kikeiyo japo kuna baadhi ya maneno ambayo huingizwa katika leksimu ya Kikeiyo bila kubadili miundo yao. Miundo ya silabi ya maneno yanapotoholewa, hubadilika kama inavyodhihirika kwenye jedwali:

**Jedwali 7: Mabadiliko ya Silabi**

| **Kiswahili** | **Kikeiyo** |
|---|---|
| [m$če$le] | [mu$če$leek] |
| [su$fu$ria] | [sa$βu$rye:t] |
| [su$ka$ri] | [su$ɣa$ru:k] |
| [ki$ko$mbe] | [ki$ɣo$mbe:t] |
| [ču$ŋvi] | [ču$mbi:k] |
| [ki$pa$nde] | [ki$βa$ndi:t] |
| [ma$ja$ni] | [ma$ča$ni:k] |


Nomino zinapokopwa katika Kikeiyo kutoka Kiswahili, hutoholewa na hivyo kupata mabadiliko katika silabi zao. Badiliko la kwanza ni la kuongezea vokali silabi ya konsonanti moja yenye usilabi inapotokea mwanzoni mwa neno kama katika:

(40 a) m$če$le > m**u$**če$leek




Neno [mčele] linabadilisha muundo wake wa kiasilia na kuchukua umbo linalokubalika na Kikeiyo. Katika silabi ya kwanza ya konsonanti yenye usilabi {m}, vokali /u/ inaongezwa kuunda silabi {mu}. Hii ni kwa sababu, Kikeiyo hakiruhusu muundo wa silabi inayoundwa kwa konsonanti pekee.


(40 b) m$ka$te > m**a$**ɣa$tiat




Katika neno [mkate], silabi ya kwanza {m} inaongezewa vokali /a/ ili kuunda silabi wazi {ma}.


Badiliko la pili la silabi ni la kurefusha vokali za silabi za mwisho kama katika:

(41 a) ču$ɱvi > ču$mbi**i**k




vokali /i/ ya neno [čuɱvi] katika silabi ya mwisho inarefushwa katika Kikeiyo. Silabi hii ya mwisho ni silabi nzito, vokali za silabi nzito hurefushwa kwa sababu ni silabi zinazowekewa mkazo.


(41 b) ma$ya$ni > ma$ča$ni**i**k




Katika neno [mayani], vokali /i/ ya silabi ya mwisho inarefushwa neno hili linapokopwa katika Kikeiyo.


Badiliko nyingine ni la kufungia silabi za mwisho kwa konsonanti. Hili hufanyika ili kuunda viambishi tamati vya wingi na umoja vya nomino. Viambishi vya umoja ni {-t}, {-et} na {-it}. Viambishi vya wingi navyo ni {-ik}, {-ok} na {ek}.

(42 a) ki$ko$mbe > ki$ɣo$mbee**t**





Silabi ya mwisho ya [kikombe] inafungiwa kwa kuongezea konsonanti. Konsonanti inapoongezwa inaunda kiambishi cha umoja {-et}.

(42 b) ča$i > ča$ii**k**





Katika neno [čai], silabi ya mwisho inafungiwa kwa kuongeza konsonanti /k/ na kuunda kiambishi {-ik} cha wingi. Ni dhahiri kutokana na mifano hii kuwa, nomino zinapokopwa hupitia mabadiliko ili zipate miundo inayokubalika na Kikeiyo. Mabadiliko hayo hubadili miundo ya silabi ya nomino asilia. Silabi nyingi za Kiswahili ni silabi wazi, silabi hizi wazi za mwisho katika neno hufungwa kwa kuongezea konsonanti. Silabi zinabadilika kwa kuongeza vokali, kurefusha vokali na kuongeza konsonanti mwishoni mwa neno ili kupata silabi pendwa ambayo ni KVK. Hata hivyo, kuna baadhi ya maneno ambayo hayabadilishi miundo ya silabi yanapokopwa. Idadi ya silabi na miundo ya silabi hizo hazibadiliki kama katika:

(43 a) [*pilau*]



(43 b) [*maɣa:*]





**3.3 Mkazo katika Nomino Mkopo za Kikeiyo**

Kiswahili na Kikeiyo ni lugha mkazo. Kama tulivyoonyesha katika 2.3.2, Kikeiyo ni lugha inayotegemea uzani wa silabi katika kuwekea maneno yake mkazo. Silabi hivyo basi, ni kiambajengo muhimu katika uchanganuzi wa mkazo wa Kikeiyo. Kikeiyo huwekea mkazo silabi nzito tofauti na Kiswahili kinachowekea mkazo silabi ya pili kutoka mwisho.

Lugha mkazo inapokopa maneno kutoka lugha mkazo nyingine, lugha pokezi husongeza mkazo wa awali katika neno linalokopwa, Kang (2010). Kikeiyo kinapokopa kutoka Kiswahili sanifu, maneno yanatoholewa. Katika utohozi, kuna mabadiliko ambayo hufanyikia silabi kama tulivyokwisha kuonyesha katika 3.2. Mabadiliko haya ya silabi hupelekea kubadilisha nafasi ya mkazo. Mkazo unahamishwa kutoka silabi ya pili kutoka mwisho hadi silabi ya mwisho ambayo ni nzito.


Kuna baadhi ya maneno ambayo hayabadilishi miundo yake yanapokopwa kwa sababu tayari yana miundo inayokubalika katika Kikeiyo. Maneno haya huhifadhi mkazo katika silabi ya pili kutoka mwisho kama katika:

(44 a) [*čaβati*]  “chapati”




Nafasi ya mkazo katika neno hili inabakia katika sehemu yake ya awali, silabi ya pili kutoka mwisho. Futi ya kimetrika ni ya kushoto. Neno hili lina silabi tatu, silabi ya kwanza {ča} ni silabi baki inayojengwa baada ya kujenga futi ya kimetrika.


(44 b) [*čela*] “jela”




Neno [jela] linaundwa kwa silabi mbili. Miundo ya silabi hizi hazibadiliki neno hili linapokopwa katika Kikeiyo. Mahali mkazo unapowekwa hivyo basi haibadiliki neno hili linapokopwa, inabakia kwenye silabi ya kwanza. Futi ya kimetrika ni ya kushoto. Hii ni tofauti na miti ya kimetrika ya maneno halisi ya Kikeiyo ambayo wakati wa kujenga, futi ni za kulia.

Katika maneno haya ambayo hayabadili miundo ya silabi, kuna maneno ambayo yana silabi nzito kama vile [maka:]. Katika nadharia ya FM, neno lolote lenye silabi nzito huwekea silabi hiyo nzito mkazo.

(44 c) [*maɣa*] “maka:”




Silabi nzito {ɣa:} katika neno [maɣa:] inapata mkazo linapokopwa. Futi ya kimetrika ni ya kulia.

Maneno mengine yanapokopwa, miundo ya silabi hubadilika kama tulivyokwisha kuona katika 3.2. Badiliko moja la silabi katika nomino mkopo za Kikeiyo ni kufunga silabi wazi za Kiswahili sanifu. Badiliko hili hupelekea silabi hizi kuwa nzito na kama tulivyoeleza, silabi nzito ni zile zenye mgao kwenye upeo silabi. Kijenzi kimojawapo cha nadharia ya FM ni kuwa, mkazo huwekwa katika silabi yoyote ambayo ni nzito. Kikeiyo, kama tulivyokwisha kuona ni lugha inayozingatia uzani wa silabi katika kuwekea mkazo maneno yake. Miundo ya silabi inapobadilika, mahali mkazo unawekwa inahamishwa kutoka silabi ya pili kutoka mwisho katika Kiswahili hadi silabi ya mwisho katika Kikeiyo ambayo ni nzito.


Kutokana na data iliyokusanywa, inaonekana kwamba isipokuwa kwa zile nomino ambazo hazibadili miundo yao ya awali, nomino nyingine zote zinafunga silabi za mwisho ambazo ni wazi.

**Jedwali 8:Mkazo Katika Nomino Zinazohesabika Katika Umoja na Wingi**

| **Nomino** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| [pen$ʹse$li] | [pen$so$ʹlit] | [pen$so$li$ʹʃek] |
| [ʹɲu$ndo] | [ɲu$ʹndu:t] | [ɲu$ndo:$ʹʃek] |
| [ʹga$ri] | [ɣa$ʹri:t] | [ɣa$ri:$ʹʃek] |
| [ʹɲa$ɲa] | [ɲa$ʹɲa:t] | [ɲa$ʹɲe:k] |
| [bu$ʹndu$ki] | [βu$ndu$ʹgi:t] | [βu$ndu$gi:$ʹʃek] |


Nomino hizi zinapokopwa ni dhahiri kuwa kuna mabadiliko yanayotokea kwenye miundo yake ya kisilabi. Mkazo unahama kutoka nafasi yake ya mwanzo, ya silabi ya pili kutoka mwisho hadi silabi ya mwisho ambayo ni silabi nzito.

(45 a) ʹɲa$ɲa > ɲa$ʹɲa:t




Neno [ɲaɲa] linapokopwa, silabi ya mwisho inawekewa mkazo tofauti na silabi ya kwanza ya neno asilia. Neno hili lina silabi moja nzito na silabi hiyo ndiyo inayopokea mkazo. Futi ya kimetrika ni ya kulia tofauti na katika Kiswahili ambapo futi ni ya kushoto.


(45 b) bu$ʹndu$ki>βu$ndu$ʹɣiit



Katika neno [bunduki], sehemu ya mkazo inabadilika kutoka silabi ya pili hadi silabi ya mwisho ambayo ni silabi nzito. Futi ya kimetrika ni ya kulia tofauti na futi ya Kiswahili, ambayo ni ya kushoto dhihiriko la kubadilika kwa nafasi ya mkazo.


Katika wingi, kuna silabi nzito zaidi ya moja katika nomino hizi. Kama tulivyoonyesha, silabi nzito zinapokuwa mbili au zaidi, mkazo unawekwa katika silabi nzito ya pili ambayo ni ya mwisho.

(46 a) [*ɣa$ri:$ʃek*] “magari”




Neno [gari] linapokopwa na kutoholewa katika wingi, silabi za pili na tatu zinakuwa silabi nzito. Silabi hizi nzito ni {ri:} yenye vokali ndefu na {ʃek} yenye koda.Mkazo unawekwa katika silabi ya mwisho {ʃek}. Futi ya kimetrika katika neno hili ni ya kulia.

(46 b) [*ɲundoʃek*] “nyundo”




Nomino [ɲundo] inapokopwa na kutoholewa katika wingi, kuna silabi mbili ambazo ni nzito. Silabi hizo ni {ndo:} na {ʃek}. Mkazo unawekwa katika silabi nzito ya mwisho {ʃek}. Futi ya kimetrika ni ya kulia.


Nomino zisizohesabika zinadhihirika katika wingi. Mifano ya nomino hizi ni *chumvi*, *sukari*, *majani*, *chai* na *mchele* katika data yetu.

**Jedwali 9: Mkazo Katika Nomino Mkopo Zisizohesabika**

| Nomino | Umbo kopwa |
|---|---|
| [ˈča$i] | [ča$ˈi:k] |
| [ma$ˈja$ni] | [ma$ča:$ˈn:ik] |
| [su$ˈka$ri] | [su$ɣa$ˈru:k] |
| [ˈču$ɱvi] | [ču:$ˈmbi:k] |
| [m$ˈče$le] | [mu$če$ˈle:k] |


Katika nomino hizi, silabi wazi za mwisho zinafungiwa na viambishi vya wingi. Silabi hizi nzito ndizo zinazopokea mkazo.

(47 a) m$ˈče$le >mu$če:$ˈle:k




Neno [mchele] linapokopwa na kutoholewa, lina silabi moja nzito ambayo ni silabi ya mwisho {le:k}. Silabi hii ya mwisho katika neno hili ndiyo inayopokea mkazo. Futi ya kimetrika ni ya kulia tofauti na katika neno asilia ambapo futi ni ya kushoto.

(47 b) čuɱvi> ču:mbi:k



Nomino [čuɱvi] inapokopwa na kutoholewa katika Kikeiyo, silabi zake zinakuwa nzito. Silabi ya mwisho ndiyo inayopokea mkazo. Futi ya kimetrika ya nomino hii ni ya kulia.

Futi za kimetrika za nomino mkopo za Kikeiyo ni za kulia. Hii ni tofauti na Kiswahili ambayo futi ni za kushoto. Badiliko la nafasi ya futi ni dhihiriko kuwa mkazo katika nomino mkopo za Kikeiyo zinabadilika kutoka nafasi za awali katika nomino asilia za Kiswahili. Nafasi ya mkazo inabadilika kutoka silabi ya pili kutoka mwisho katika Kiswahili hadi silabi nzito ya mwisho katika Kikeiyo. Badiliko hili ni kutokana na kubadilika kwa miundo ya silabi za nomino mkopo katika Kikeiyo wakati wa utohozi.


### 3.4 Toni za Nomino Mkopo za Kikeiyo

Kiswahili sanifu si lugha toni tofauti na Kikeiyo ambayo kama tulivyoonyesha katika 2.3.3 ni lugha toni. Kikeiyo kinatumia sifa ya toni katika kutofautisha maana za maneno na pia katika kubainisha kategoria za maneno. Nomino za Kiswahili sanifu hutamkwa kwa toni kati, utamkaji wa silabi zao zinahusisha utamkaji ambao si wa chini wala si wa juu. Nomino hizi zinapokopwa katika Kikeiyo, zinatoholewa ili ziambatane na mifumo ya kifonolojia ya Kikeiyo na hivyo kupata sifa ya toni.

Kikeiyo kama ilivyokwisha kubainishwa katika 2.3.3 kina aina tano za toni ambazo ni toni kati, toni chini, toni juu, toni panda na toni shuka. Toni hizi hudhihirika kwa namna mbalimbali kutegemea miundo ya silabi na pia kutegemea maana msemaji anataka kuwasilisha iwapo ni katika kutofautisha maana za maneno yanayofanana.

Nomino zinapokopwa katika Kikeiyo, huongezewa viambishi vya idadi. Nomino ni za maumbo mawili, nomino msingi na nomino za upili. Nomino msingi huchukua viambishi {-t}, {-in} na {ɵ} katika umoja na {-in}, {-on} na {-oi} katika wingi. Viambishi hivi hubeba toni za aina tofauti, Chelimo n.w (2015).

Katika utafiti wetu tulitumia kichanganuzi kidatu cha Praat kuchanganulia toni. Sauti zilirekodiwa na kisha kasimawimbi zikaonyeshwa kwenye michoro. Nomino mkopo [*nyuɣu:k*] kwa mfano, ilipotamkwa silabi zilitamkwa kwa kasimawimbi kama inavyojitokeza katika mstari uliokolezwa kwenye mabano kwenye mchoro:




Kutokana na kasimawimbi hii, iliwezekana kuona kidatu kilivyojitokeza katika silabi. Kwa mfano, kidatu katika neno hili ni ya chini ikipanda kumaanisha ni toni panda ambapo vokali /u/ ya silabi ya kwanza inatamkwa kwa toni chini na vokali /u:/ ya silabi ya pili kwa toni juu. Kimatawi, nomino hii inawakilishwa:

(48) [*nyugu:k*] "njugu"

Rusu ya fonimu ny u g u k

Rusu ya KV K V K V V K

Rusu ya toni C J

Tulifanya hivi katika nomino zote.

**Jedwali 10: Toni za Nomino Mkopo za Maumbo ya Kimsingi**

| **Nomino** | **Umbo msingi, umoja** | **Umbo msingi, wingi** |
|---|---|---|
| [mkate] | [màɣatjá] | [màɣatíín] |
| [meza] | [méésò] | [méésoʃaí] |
| [paŋga] | [pàŋgaí] | [pàŋgaín] |
| [sufurja] | [sàβurió] | [sàβuríóón] |
| [čai] | | [čàín] |

Katika nomino za kimsingi zenye kuundwa kwa silabi mbili, silabi ya kwanza ni ya toni kati isipokuwa pale silabi ya kwanza ni silabi nzito. Silabi inapokuwa nzito

hutamkwa kwa toni juu. Silabi ya pili katika nomino zenye silabi mbili huchukua toni chini kama katika:

(49 a) [*méésò*] "meza"

Rusu ya fonimu m e s o
Rusu ya KV K V V K V
Rusu ya toni J C

Neno [*méésò*] linaundwa kwa silabi mbili. Silabi ya kwanza ni nzito kwa sababu ina vokali refu /e:/. Silabi hii hivyo basi, inatamkwa kwa toni juu. Silabi ya pili ni ya toni chini.

(49 b) [*pàŋgaí*] "panga"

Rusu ya fonimu p a ŋg ai
Rusu ya KV K V K V
Rusu ya toni C J

Nomino [*pàŋgaí*] inaundwa kwa silabi mbili. Vokali ya silabi ya kwanza ni ya toni chini. Silabi ya pili ni silabi nzito kwa sababu inaundwa kwa irabu-unganifu /ai/. Silabi hii ni ya toni juu.

Nomino zenye kuundwa kwa zaidi ya silabi mbili huwa na mfuatano wa toni chini kati juu (CKJ) kama katika:

(50 a) [*mà$ɣa$tjá*] "mkate"

Rusu ya fonimu m a ɣ a t y a
Rusu ya KV K V K V K KV
Rusu ya toni C K J

Nomino [*mà$ɣa$tjá*] ina silabi tatu. Vokali /a/ ya silabi ya kwanza ni ya toni chini. Vokali /a/ ya silabi ya pili ni ya toni kati na vokali /a/ ya silabi ya mwisho ni ya toni juu.

(51 b) [*sàβurió*] “sufuria”

Rusu ya fonimu s à β u r ió

Rusu ya KV K V K V K V

Rusu ya toni C K J

Neno [*sàβurió*], lina mfuatano wa toni chini kati juu sawa na nomino asilia za Kikeiyo zenye kuundwa kwa silabi tatu.

Viambishi vya wingi vya maumbo ya kimsingi hubeba toni za aina tofauti kama ilivyokwisha kuonyeshwa katika 2.3.3. Kiambishi {-in} ni cha toni juu ilhali {-on} ni cha toni chini. Kiambishi {-on} hata hivyo, huweza kuwa toni juu kinapounganishwa na vokali nyingine ya mzizi wa nomino na kufanya iwe nzito kama katika:

(52 a) [*sàburióón*] “sufuria”

Rusu ya fonimu s a b u r io o n

Rusu ya KV K V K V K V V K

Rusu ya toni C K J

Kiambishi {-on} kinaunganishwa na vokali /o/ ya toni kati. Vokali /o/ inakuwa refu na hili linapelekea toni hii ya kati kuwa ya toni juu.

Kiambishi {-in} kinabeba toni juu kwa sababu vokali /i/ ni vokali ya juu na vokali za juu hubeba toni juu kama katika:

(52 b) [*màɣatíín*] “mikate”

Rusu ya fonimu m a ɣ a t i i n

Rusu ya KV K V K V KV V K

Rusu ya toni C K J

Nomino [*màɣatíín*] ina kiambishi {-in} yenye kubeba toni juu.

Maumbo ya upili ya nomino mkopo ndio maumbo yanayotumiwa sana katika mawasiliano kutokana na data iliyokusanywa. Katika umoja, nomino zinaongezewa viambishi {-it}, {-et} na {ɵ}. Viambishi vya wingi ni {-ik},{-ek} na {-ok}. Viambishi vya wingi hubeba toni tofauti. Kiambishi {-ik} ni cha toni juu, kiambishi {-ek} ni cha toni kati na {-ok} ni cha toni chini.

**Jedwali 11: Toni za Nomino Mkopo za Kikeiyo za Maumbo ya Upili**

| **Nomino** | **Nomino katika umoja** | **Nomino katika wingi** |
|---|---|---|
| [ndizi] | [ndìʃót] | [ndìsííník] |
| [bakuli] | [bàɣulíít] | [βàɣulííʃék] |
| [ta:] | [tááìt] | [tááííʃék] |
| [kitabu] | [kìtabùùt] | [kìtaβúʃék] |
| [kičana] | [kìpčanúéét] | [kìpčanúóók] |
| [stima] | [sítíméét] | [sìtímóók] |

Katika nomino za umoja zinazoundwa kwa silabi mbili, silabi ya kwanza ni ya toni chini isipokuwa pale silabi ya kwanza ni silabi nzito na hivyo kuwa ya toni juu. Silabi ya pili ya nomino hizi ni za toni juu. Katika jedwali (11), maneno [*ndìʃót*] "ndizi" na [*tááìt*] "taa" yana miundo ya silabi mbili. Toni za silabi hizi zinadhihirika kwa namna tofauti kama ifuatavyo:

(53 a) [*ndìʃót*] "ndizi"

Rusu ya fonimu nd i ʃ o t
Rusu ya KV K V K V K
Rusu ya toni C J

Vokali /i/ katika nomino [ndiʃot] ni vokali ya juu lakini inatamkwa kwa toni chini. Vokali /o/ ni vokali ya kati lakini inatamkwa kwa toni juu. Hii ni kwa sababu vokali

za kwanza kwa nomino za maneno ya silabi mbili hutamkwa kwa toni chini na ya pili kwa toni juu bila kuzingatia sifa za vokali husika.

(53 b) [*ta:it*] “taa”

Rusu ya fonimu t a i t
Rusu ya KV K VV V K
Rusu ya toni J J

Katika neno [*ta:it*], silabi ya kwanza ni ya toni juu kwa sababu ina silabi nzito yenye vokali refu. Silabi ya pili pia ni ya toni juu kwa sababu ni silabi nzito. Silabi hii ya pili ndiyo inayowekewa mkazo.

Katika wingi, nomino zina viambishi vya aina tatu za wingi. Viambishi hivi vinabeba toni tofauti. {-ik} ni ya toni juu kama katika:

(54 a) [*ndìsííník*] “ndizi”

Rusu ya fonimu nd i s i n i k
Rusu ya KV K V K V V K V K
Rusu ya toni C J

(54 b) [*kitu:ŋgui:k*] “vitunguu”

Rusu ya fonimu k i t u ŋg u i k
Rusu ya KV KV K VV K V V V K
Rusu ya toni C J J J

Kiambishi {-ek} ni cha toni kati lakini katika jedwali (11), kiambishi hiki ni cha toni juu. Hii ni kwa sababu, kiambishi hiki kinaambatanishwa na vokali nyingine za mzizi wa nomino na kufanya vokali /e/ kuwa ndefu. Vokali zinapokuwa ndefu hufanya silabi kuwa nzito. Silabi nzito hupokea mkazo. Silabi zinazopokea silabi hutamkwa kwa toni juu. Katika nomino [*kìtaβúúʃék*] “vitabu” na [*βàɣulííʃék*] “bakuli”, inaonekana kuwa kiambishi hiki ni cha toni juu:

(55 a) [*kìtaβúúʃék*] "vitabu"

| | |
|---|---|
| Rusu ya fonimu | k i t a β u ʃ e k |
| Rusu ya KV | K V K V K V V K V K |
| Rusu ya toni | C K J |

(55 b) [*βàɣulííʃék*] "bakuli"

| | |
|---|---|
| Rusu ya fonimu | β a ɣ u l i ʃ e k |
| Rusu ya KV | K V K V K V V KV K |
| Rusu ya toni | C K J |

Nomino (55) zina silabi nne na miundo ya toni za mpandashuko za chini kati juu. Silabi ya mwisho ni kiambishi cha wingi {-ek} chenye toni juu tofauti na hali yake asilia ya kuwa kiambishi cha toni kati. Hili linatokana na hali kuwa ni viambishi vya idadi vinavyopata mkazo. Silabi zinazopata mkazo bila kuzingatia sifa ya vokali zao huwa za toni juu.

Kiambishi cha wingi {-ok} kwa kawaida ni cha toni kati lakini katika jedwali (11), kiambishi hiki ni cha toni juu. Hii ni kwa sababu kiambishi hiki kinaambatanishwa na vokali nyingine za mzizi wa nomino na kufanya vokali /o/ kuwa ndefu. Vokali zinapokuwa ndefu hufanya silabi kuwa nzito. Silabi nzito hupokea mkazo. Silabi zinazopokea mkazo hutamkwa kwa toni juu.

(56 a) [*kìpčanúóók*] "vichana"

| | |
|---|---|
| Rusu ya fonimu | k i p č a n uo o k |
| Rusu ya KV | K V K K V K V V K |
| Rusu ya toni | C K J |

(56 b) [*sìtímóók*] "stima"

| | |
|---|---|
| Rusu ya fonimu | s i t i m o k |
| Rusu ya KV | K V KV K V V K |
| Rusu ya toni | C J J |

Katika nomino (62), kiambishi cha wingi {-ok} ni cha toni juu kwa sababu kinaandamana na vokali /o/ ya mzizi wa neno na hivyo kufanya silabi kuwa nzito na ya toni juu.

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kuwa nomino zinapokopwa kutoka Kiswahili sanifu hupokea sifa ya toni katika silabi zake. Hii ni tofauti na nomino hizi kiasilia kwa sababu Kiswahili sanifu si lugha toni. Inaonekana pia kuwa silabi zinazowekewa mkazo huathiri toni ya silabi hiyo. Silabi zinazowekewa mkazo zinatamkwa kwa toni juu. Viambishi vya umoja na wingi vinavyoongezewa nomino mkopo huathiri miundo ya toni katika nomino hizo.

## 3.5 Hitimisho

Katika sura hii, tumeonyesha sifa za kiarudhi za nomino mkopo za Kikeiyo. Nomino zinapokopwa katika Kikeiyo, hutoholewa. Utohozi unahusisha mabadiliko ya miundo ya silabi inabadilika. Miundo ya silabi inapobadilika, mahali mkazo unawekwa unabadilika. Inaonekana kuwa mkazo upo katika silabi ya mwisho ambayo ni nzito. Hii ni ishara kuwa uzani wa silabi unaathiri mahali mkazo unawekwa katika nomino mkopo. Nomino mkopo zinapata sifa ya toni. Mfumo wa toni za Kikeiyo unadhihirika katika nomino mkopo.

# SURA YA NNE

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 Utangulizi

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuthibitisha kuwa nomino zinapokopwa katika Kikeiyo kutoka Kiswahili, hupokea sifa za kiarudhi za Kikeiyo. Tulichanganua sifa za kiarudhi za nomino mkopo za Kikeiyo. Nadharia za fonolojia vipandesauti huru na fonolojia mizani zilitumiwa kutekeleza uchanganuzi huu. Nadharia ya fonolojia vipandesauti huru ilitumika kuelezea miundo ya silabi za Kikeiyo na kuchanganua sifa ya toni katika nomino mkopo za Kikeiyo. Nadharia ya fonolojia mizani ilitumika kuchanganua sifa ya mkazo katika Kikeiyo na namna mkazo unavyojitokeza katika nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili sanifu. Sura hii inatoa muhtasari, matokeo na mapendekezo ya utafiti wetu.

## 4.2 Mahitimisho

Uchunguzi huu ulijikita katika uchanganuzi wa sifa za kiarudhi za Kikeiyo katika nomino mkopo kutoka Kiswahili sanifu. Sifa za kiarudhi zilizochanganuliwa ni sifa za mkazo, toni na silabi.

Katika sura ya kwanza, tulishughulikia maswala ya kimsingi yanayojenga utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti yanayochochewa na malengo hayo, sababu zilizopelekea kuchaguliwa kwa mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu lugha za Kalenjin na fonolojia arudhi, misingi ya nadharia zilizoongoza utafiti huu na mbinu zilizotumika katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data.

Utafiti wetu ulilenga kujibu maswali matatu ya utafiti. Tulitaka kujua ni sifa zipi za kiarudhi zinazopatikana katika Kikeiyo. Katika sura ya pili, tulijadili sifa za kiarudhi zinazopatikana katika Kikeiyo. Sifa hizi ni sifa za silabi, mkazo na toni katika Kikeiyo. Tuliweza kuthibitisha kuwa Kikeiyo kina silabi wazi na funge. Silabi wazi ni

zile zinazoishia kwa vokali na silabi funge ni zile zilizo na koda. Silabi pendwa katika Kikeiyo ni silabi KVK na KV. Tulielezea pia mkazo unavyojitokeza katika Kikeiyo. Tuliona kuwa Kikeiyo kina mkazo changamani. Mkazo changamani ni ule unaotegemea uzani wa silabi. Ilibainika kuwa Kikeiyo huwekea silabi nzito mkazo. Katika Kikeiyo, futi za kimetrika ni za kulia. Hii ina maana kuwa mkazo unawekwa kwenye silabi ya mwisho na silabi hizi huwa nzito. Silabi katika Kikeiyo ina jukumu la kifonolojia la kuonyesha idadi ya nomino. Mwisho, tulichanganua sifa ya toni katika Kikeiyo. Tuliona kuwa kuna aina tano za toni ambazo ni; toni kati, toni juu, toni chini, toni panda na toni shuka. Toni hudhihirika kwa namna tofauti katika nomino za msingi na nomino za upili. Sifa mbalimbali za vokali huathiri toni za vokali hizo kwa mfano, vokali za juu ni za toni juu. Hata hivyo, hili linaweza kukiukwa kutegemea miundo ya silabi. Silabi nzito zenye vokali ndefu kwa mfano, ni za toni juu hata kama vokali ni za chini. Silabi zinazowekewa mkazo zinatamkwa kwa toni juu. Toni katika Kikeiyo ina majukumu ya kileksika katika kutofautisha maana za maneno na kisarufi katika kubainisha kategoria za maneno.

Kiswahili na Kikeiyo zina sifa tofauti za kiarudhi. Nomino zinapokopwa kutoka Kiswahili, hulazimika kutoholewa ili ziingie katika mifumo ya kifonolojia ya Kikeiyo. Utohozi huu huathiri miundo ya silabi kama tulivyokwisha kuonyesha katika sura ya tatu. Miundo ya silabi za nomino mkopo hubadilika kwa kuongezea silabi za konsonanti pekee vokali. Hii ni kutokana na Kikeiyo kutokuwa na silabi za konsonanti pekee. Badiliko jingine ni la kufungia vokali wazi kwa konsonanti hasa silabi za mwisho. Silabi za mwisho huwa na viambishi vya idadi. Badiliko la mwisho ni la kurefusha wakaa wa vokali. Mabadiliko haya ya miundo ya silabi hupelekea kusongezwa kwa nafasi ya mkazo kutoka silabi ya pili kutoka mwisho hadi silabi ya mwisho ambayo ni silabi nzito. Suala letu la pili la utafiti linajibiwa kwamba miundo

ya silabi za Kikeiyo huathiri mahali mkazo unawekwa. Hata hivyo, sio nomino zote zinatoholewa katika Kikeiyo. Kuna nomino zinazoingizwa katika leksimu ya Kikeiyo bila kubadili miundo yao ya silabi kwa sababu zina miundo inayokubalika katika Kikeiyo. Iwapo hivyo, nafasi ya mkazo inabaki katika silabi ya pili kutoka mwisho.

Mwisho,tulitaka kujua iwapo nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili zinapata sifa ya toni kwa sababu, Kiswahili tofauti na Kikeiyo ni lugha isiyokuwa ya toni Ilithibitishwa kuwa nomino za Kiswahili zinapoingizwa katika Kikeiyo, hupokea sifa ya toni. Nomino hizi zilichukua miundo ya toni za Kikeiyo. Nomino katika umbo la kimsingi lenye silabi mbili zina toni mbili, toni ya silabi ya kwanza ni ya kati na ya silabi ya pili ni ya chini. Maumbo haya yanapokuwa ya upili, toni kati ya silabi ya kwanza inabadilika na kuwa ya chini. Toni chini ya silabi ya pili nayo inabadilika na kuwa toni ya juu. Nomino zinapokuwa na silabi tatu na zaidi, silabi ya kwanza ni ya toni chini, silabi ya pili ya toni kati na silabi ya tatu ya toni juu. Toni ya silabi ya tatu husambaa kwa silabi nyingine zinazokuja baada yake.

### 4.3 Mapendekezo

Utafiti wetu umeonyesha kwamba nomino zinapokopwa kutoka Kiswahili sanifu kuna mabadiliko ya silabi ambayo hutokea. Badiliko moja la silabi ni kurefusha vokali. Hili ni dhihiriko la kuwepo kwa sifa ya wakaa katika Kikeiyo. Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha sifa ya wakaa katika nomino mkopo za Kikeiyo kutoka Kiswahili.

Utafiti wetu umeshughulikia nomino pekee. Utafiti unapaswa kufanyiwa kategoria nyingine za maneno mkopo kama vile vitenzi na vivumishi na kuona namna sifa za kiarudhi zinavyojitokeza katika kategoria hizi za maneno.

Nomino zilizotafitiwa ni zile zinazotokana na Kiswahili sanifu. Kikeiyo ni lugha inayopakana na lugha nyingine kama vile Kimarakwet, Kiingereza, Kinandi na Kitugen. Kuna haja ya kutafitia nomino mkopo za Kikeiyo zinazotokana na lugha hizi na kuona athari za sifa za kiarudhi za Kikeiyo kwa nomino hizo.

## MAREJELEO


Akida, M. A. (2013). Phonological and Semantic Change in Language Borrowing: The Case of Arabic Words Borrowed into Kiswahili katika *International Journal of Education and Research* vol. 1 No. 4.

Arlotto, A. (1972). *Introduction to Historical Linguistics*. Boston: Houghton Mifflin Company.

Bendor-Samuel, J. T. (1966). Some Prosodic Features in Terena katika *in Memory of J. R. Firth.*ed. Bazell, C. E. Catford, J. C. Halliday, M. A. K &Robins, R. H. (1966). London: Longman Group Ltd.

Bloomfield, L. (1933). *Language History.* New York: Holt, Rinehart and Winston, Inc.

Boen, P. C. (2014). Loan Words in Nandi from English and Kiswahili Languages. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Bynon, T. (1977). *Historical Linguistics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Chege, S. N. (2009). Morphonological Modifications of English and Kiswahili Loanwords in Maasai. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Chelimo, A. K. & Randich, J. C. (2014). The Systemmatic Phonological Realization in Kiyo Language as Spoken by the Keiyo Community in Kenya katika *International Journal of Humanities and Social Sciences* vol 4 No.6.

Chelimo, A. K., Chepkirui, J. & Kibet, J. (2015). Effects of Plural Suffixation on Tone Assignmnt in Keiyo Language Spoken by the Keiyo Community in Kenya katika *Research on Humanities and Social Scinces* Vol. 5 No. 15.

Chomsky, N. & Halle, M. (1968). *Sound Patterns of English.* New York: Harper and Row.

Clark, J. & Yallop, C. (1995). *An Introduction to Phonetics and Phonology*. Oxford: Blackwell Publishers Ltd.

Clements, G. N. & Keyser, S. J. (1983). *CV Phonology: A Generative Theory of the Syllable.* Massachusetts: MIT.

Creider, C. A. (1982). *Studies in Kalenjin Nominal Tonology.* Berlin: Dietrich Reimer Verlag.

Crystal, D. (2000). *Language Death.* Cambridge: Cambridge University Press.

Firth, J. R. (1934-1951). *Papers in Linguistics.* London: Oxford University Press.

Fox, A. (2000). *Prosodic Features and Prosodic Structure: The Phonology of Suprasegmentals.* New York: Oxford University Press, Inc.

Fromkin, V. Rodman, R & Hyams, N. (2003). *An Introduction to Language* 7th edition. Massachusetts: Thomson Corporation.

Garde, P. (1967). Principles of the Synchronic Description of Stress katika *Phonology.* Ed. Fudge, E. C. (1973). Harmondsworth: Penguin Books.

Goldsmith, J. A. (1976). *Autosegmental Phonology*. Bloomington: Indiana University Linguistics Club.

Goldsmith, J. A. (1990). *Autosegmental and Metrical Phonology*. Oxford: Basil Blackwell

Hayes, B. (1988). *A Metrical Theory of Stress Rules*. Bloomington: Indiana University Linguistics Club.

Hockett, C. F. (1958). *A Course in Modern Linguistics*. Canada: The Macmillan Company.

Hogg, R. & McCully, C. B. (1987). *Metrical Phonology*. Cambridge: Cambridge University Press.

Hulst, H. & Smith, N. (1982). *The Structure of Phonological Representations.* Holland: Foris Publications.

Hyman, L. M. (1975). *Phonology: Theory and Analysis*. New York: Holt, Rinehart and Winston.

Hyman, L. M. (2003). *A Theory of Phonological Weight*. Stanford: Center for the study of Language & Information.

Iribemwangi, P. I. (2010). *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound Changes and Words*. Brücken: VDM Verlag.

Jerono, P. (2012). *Tugen Word Order: A Minimalist Perspective.* Kocani: Egalite publishers.

Kandagor, M. & Sawe, S. (2014). Resyllabification of Loan Words in Kalenjin Phonology katika *Research on Humanities and Social Sciences* Vol. 4 No. 6.

Kang, Y. (2010). Suprasegmental Adaptation in Loanwordsretrieved fromwww.elsevier.com/locate/lingua.

Kenstonwicz, M. & Kisseberth, C. (1979). *Generative Phonology: Description and Theory*. New York: Academic Press, INC.

Koske, (2006). Vowel Harmony In Kipsigis: An Autosegmental phonological Theory Approach. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi ambayo haijachapishwa.

Ladefoged, P. (1982). *A Course in Phonetics.* San Diego: Harcourt Brace Jovanovich publishers Inc.

Lass, R. (1988). *Phonology: An Introduction to Basic Concepts.* Cambridge: Cambridge University Press.

Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoretical Linguistics*. New York: Cambridge University Press.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo Katika Nadharia ya Fonolojia.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2012). *Misingi ya Fonolojia.* Dar es Salaam: TUKI.

Milroy, L. (1987). *Observing and Analyzing Natural Language: A Critical Account of Sociolinguistic Method.* New York: Basil Blackwell Inc.

Mbaabu, I. (1991). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili.* Nairobi: Longman Publishers.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mutiga, J. M. (2002). The Tone System of Kikamba: A Case Study of Mwingi Dialect. Tasnifu ya uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mwaliwa, H. C. (2014). An Analysis of the Syllable Structure of Standard Kiswahili Loanwords from Modern Standard Arabic. Tasnifu ya uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mweri, J. (2010). *Utangulizi wa Isimu.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Nathan, G. S. (2008). *Phonology: A Cognitive Grammar Introduction.* Amsterdam: John Benjamins Publishing Company.

Oduor, J. A. N (2002). A Study of Syllable Weight and its Effects in Dholuo Phonology. Tasnifu ya uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

O'Grady. W., Dobrovolsky, M. & Katamba, F. (1997). *Contemporary Linguistics: An Introduction.* Harlow: Addison Wesley Longman Ltd.

Pike, K. L. (1948). *Tone Languages: A Technique for Determining the Number and Type of Pitch Contrasts in a Language with Studies in Tonemic Substitution and Fusion.* Michigan: The University of Michigan Press.

Sapir, E. (1921). *Language: An Introduction to the Study of Speech.* New York: Harcourt, Brace and world.

Tarus, I. (1994). The Keiyo of Kenya during the Early Colonial Period (1902-1939). Tasnifu ya uzamifu ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Toweett, T. (1975). Kalenjin Nouns and their Classification.Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Verma, S. K. &Krishnaswamy, N. (1989). *Modern Linguistics: An Introduction.* Delhi: Oxford University Press.

Wachera, S. K. (2008). Tone as a Distinctive Lexical Feature in the Lexicon of Gi-Gichugu Dialect, Gikuyu Language. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Whiteley, W. H. (1974). The Classification and Distribution of Kenya's African Languages katika *Languages in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

Yamo, J. O. (2014). Loanword Adaptation in Boro-Ukwala Dialect of Dholuo: A Case Study of Borrowing from Lumarachi, Lunyala and Kiswahili. Tasnifu ya uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Yip, M. (2002). *Tone.* Cambridge: Cambridge Univeristy Press.

## KIAMBATISHO

## MANENO MKOPO YA KIKEIYO KUTOKA KISWAHILI SANIFU

Orodha ifuatayo ya nomino mkopo sabini na tisa za Kikeiyo kutoka Kiswahili sanifu ndiyo ilitumika kukusanyia data ya utafiti huu.

| | **Kiswahili** | **Kikeiyo, umoja** | **Kikeiyo, wingi** |
|---|---|---|---|
| 1 | [mčele] | | [mučele:k] |
| 2 | [tunda] | [matundia:t] | [matunde:] |
| 3 | [maharagwe] | | [marakwe:k] |
| 4 | [njugu] | | [injugu:k] |
| 5 | [čapati] | [čaβati] | [čaβati:ʃek] |
| 6 | [ndizi] | [ndiʃo:t] | [ndisi:nik] |
| 7 | [čai] | | [čai:k] |
| 8 | [majani] | | [mačani:k] |
| 9 | [viazi] | [pjasiat] | [pjasi:nik] |
| 10 | [ɲaɲa] | [ɲaɲa:t] | [ɲaɲe:k] |
| 11 | [kituŋgu:] | [kitu:ŋgu:ot] | [kitu:ŋguik] |
| 12 | [sukari] | | [suɣaru:k] |
| 13 | [čumvi] | | [čumbi:k] |
| 14 | [bakuli] | [βaɣuli:t] | [βaɣuli:ʃek] |
| 15 | [sahani] | [sa:ni:t] | [sa:ni:ʃek] |
| 16 | [mkebe] | [muɣebe:t] | [muɣeβe:ʃek] |
| 17 | [ndo:] | [ndo:it] | [ndo:i:ʃek] |
| 18 | [kijiko] | [kičiɣe:t] | [kičiɣoi:k] |
| 19 | [kikombe] | [kiɣo:mbe:t] | [kiɣo:mboi:k] |
| 20 | [sufuria] | [saβurie:t] | [saβurio:nik] |
| 21 | [birika] | [kiβiriɣe:t] | [kiβiriɣo:k] |
| 22 | [uma] | [u:mait] | [ume:ʃek] |
| 23 | [kichuŋgi] | [kičuŋgi:t] | [kičuŋgi:ʃek] |
| 24 | [kiberiti] | [kiβiriti:t] | [kiβiriti:ʃek] |
| 25 | [sabuni] | [saβuni:t] | [saβuni:ʃek] |
| 26 | [kabati] | [kaβatit] | [kaβati:nik] |
| 27 | [taa] | [ta:i:t] | [ta:i:ʃek] |
| 28 | [meza] | [mese:t] | [meso:ʃek] |
| 29 | [karai] | [kara:it] | [karai:ʃek] |
| 30 | [kufuli] | [kuβuli:t] | [kiβuli:ʃek] |
| 31 | [čupa] | [čuβe:t] | [čuβa:i:k] |
| 32 | [stima] | [sitime:t] | [sitimo:k] |
| 33 | [maka:] | [maɣa:] | [maɣa:ek] |
| 34 | [mfuko] | [maβuge:t] | [maβuɣo:ʃek] |
| 35 | [karatasi] | [karta:sit] | [kartasi:nik] |
| 36 | [kitabu] | [kitaβu:t] | [kitaβu:ʃek] |
| 37 | [kalamu] | [kala:mit] | [kalami:ʃek] |
| 38 | [mpira] | [mbi:re:t] | [mbiro:k] |
| 39 | [penseli] | [pe:nselit] | [pensoli:ʃek] |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 40 | [kiɲozi] | [kiɲosi] | [kiɲosi:ʃek] |
| 41 | [mabati] | [kiβatit] | [kiβati:nik] |
| 42 | [dirisha] | [tiriʃeet] | [tiriʃo:k] |
| 43 | [ŋgazi] | [iŋgasit] | [ŋgasi:ʃek] |
| 44 | [msumari] | [kipčumaria:t] | [kipčumari:k] |
| 45 | [panga] | [pa:ŋge:t] | [paŋgai:k] |
| 46 | [hema] | [e:mait] | [e:mai:nik] |
| 47 | [ɲundo] | [ɲundu:t] | [ɲundui:nik] |
| 48 | [mbao] | [paoiyo:t] | [paoi:nik] |
| 49 | [mtaimbo] | [tarimboit] | [tarimboin] |
| 50 | [makasi] | [maɣasit] | [maɣasi:nik] |
| 51 | [sindano] | [sindanu:t] | [sindanu:ʃek] |
| 52 | [leso] | [le:soit] | [lesoi:nik] |
| 53 | [kitamba:] | [kitambae:t] | [kitambao:k] |
| 54 | [simu] | [sime:t] | [si:me:ʃek] |
| 55 | [redio] | [retioit] | [retioi:nik] |
| 56 | [gari] | [ɣari:t] | [ɣari:ʃek] |
| 57 | [pasi] | [pa:sit] | [pasi:nik] |
| 58 | [ufuŋguo] | [kiβu:ŋgue:t] | [kiβuŋguo:k] |
| 59 | [jela] | [če:la] | [če:la] |
| 60 | [kipande] | [kiβa:ndit] | [kiβa:ndi:nik] |
| 61 | [kitana] | [kipčanue:t] | [kipčanuo:k] |
| 62 | [kura] | [kuraiya:t] | [kurai:nik] |
| 63 | [serikali] | [seriɣali:t] | [sergali:ʃek] |
| 64 | [gazeti] | [ɣase:ti:t] | [ɣaseti:nik] |
| 65 | [kipindi] | [kiβi:ndi] | [kiβindi:ʃek] |
| 66 | [askari] | [askari:ndet] | [askari:k] |
| 67 | [daktari] | [taktari:n] | [taktari:nik] |
| 68 | [mwalimu] | [mwalimuiyo:t] | [mwalimui:nik] |
| 69 | [ndege] | [ndege:t] | [ndege:ʃek] |
| 70 | [baisikeli] | [ba:skilit] | [baskili:nik] |
| 71 | [dereva] | [ndereβai:n] | [ndereβai:nik] |
| 72 | [barua] | [paruwe:t] | [βaruwe:ʃek] |
| 73 | [filimbi] | [siri:mbit] | [sirimbi:nik] |
| 74 | [jumamosi] | | [čuma:mos] |
| 75 | [jumapili] | | [čuma:mbili] |
| 76 | [kanisa] | [kani:sa] | [kani:so:ʃek] |
| 77 | [kibeti] | [kaβeti:t] | [kaβeti:nik] |
| 78 | [msalaba] | [musalaβe:t] | [musalaβe:ʃek] |
| 79 | [bunduki] | [punduɣi:t] | [punduɣi:ʃek] |